

**REPUBLIC OF KENYA**  
**MACHAKOS COUNTY ASSEMBLY**

**OFFICIAL REPORT**

**Wednesday, 23<sup>rd</sup> June, 2021**

**Special Sitting**

*(Convened via Kenya Gazette Notice No.5899  
(Vol. CXXIII—No. 133 of 18th June, 2021)*

The House met at 11.48 a.m.

*[The Speaker (Hon. (Mrs.) Mwangangi) in the Chair]*

**PRAYERS**

**COMMUNICATIONS FROM THE CHAIR**  
**CONVENTION OF BUNGE MASHINANI SITTING AT KOLA WARD**

**Hon. Speaker:** Hon. Members, under this Order, I have the following communication to make. The first one is on *Bunge Mashinani*, that is what we are having right now. Hon. Members of the County Assembly of Machakos, ladies and gentlemen, I welcome you all to this sitting which is the fifth forum of *Bunge Mashinani*. This *Bunge Mashinani* forum has been organized to help to ensure the realization of the national values and principles of governance that are outlined in Article 10 of the Constitution of Kenya, as well as the attainment of the objects and principles of devolution as provided for under Article 174 of the Constitution.

Hon. Members, Article 196(1) of the Constitution provides that a County Assembly shall conduct its business in an open manner and hold its sittings and those of its committees in public and facilitate public participation and involvement in the legislative and other business of the Assembly and its committees. In this light, the County Assembly resolved to hold two *Bunge Mashinani* forums in each Sub-County.

This is the fifth such forum having had the inaugural *Bunge Mashinani* in Yatta Sub-County at Kithimani Ward on 17<sup>th</sup> October, 2018, the second one being held in Masinga Sub-County at Ndithini Ward on 15<sup>th</sup> May, 2019, the third one in Mwala Sub-County at Kibauni Ward on 4<sup>th</sup> December, 2019 and the fourth one in Matungulu Sub-County at Kyeleni Ward on 29<sup>th</sup> September, 2020.

You recall that the country and the whole world got the infection of the coronavirus which affected our physical interaction through *Bunge Mashinani* and so we had to take a back step in the process to safeguard the public and members of staff that are involved in *Bunge Mashinani*. Hon. Members, I will address you more on the issue of Covid-19 public health protocols as we go on.

On convening of this sitting, you remember we vide Gazette Notice No.5899 (Vol. CXXIII—No. 133) issued on 18th June, 2021 advertised for this sitting. The Notice gave Members of the County Assembly of Machakos and the general public information that pursuant to Article 10(2)(a), 74 and 196 of the Constitution as read with Sections 87, 91(g), 98(1) and 99 of the County Governments Act, 2012, the County Assembly of Machakos shall hold its sittings of the 23<sup>rd</sup> June, 2021 at Katuaa Market, Kola Ward, Machakos Town Sub-County, Machakos County.

During the said sitting, the Assembly shall conduct its regular business in plenary sitting as per the County Assembly of Machakos Calendar (Regular Sessions) for the Fifth Session, 2021. The matters to be deliberated during the said sitting shall be as may be determined according to Standing Order 151(5)(d), (e) and (f) of the County Assembly of Machakos Standing Orders. Accordingly, this is to notify all Members of the County Assembly of Machakos and the general public that the sittings of the day shall commence at 10.00 a.m. and the second sitting at 2.30 p.m.

Apologies Hon. Members, we are starting a little late because you appreciate the logistics of planning for a sitting outside the Assembly so there has been a slight delay on the commencement of the morning sitting.

#### OBJECTIVES OF THE BUNGE MASHINANI SITTING

Hon. Members, you recall we have principles of devolution of taking services close to and this Assembly is wake to that requirement and the purpose is to reach members of the county of Machakos who are not able to travel to the Assembly premises to watch hand lists as you conduct your business.

So in this sitting the public will have an opportunity to see how business in the Assembly is conducted and also be able to understand the role of their Member of County Assembly in the County.

This forum will also accord all members of the public particularly in this ward, an opportunity to share with the Members of the Assembly led by Hon. Eric Musembi who is the member of this ward and they will also interact with the members on any matter that they wish the Assembly to undertake on their behalf in the execution of the mandate of the Assembly.

So Hon. Members, give your ears when it is time for the members of the public present so that you can address their issues on a one-to-one basis. Through this forum, it is expected that the public can also originate, through interaction with the Hon. Members, Bills on matters that require to be addressed in their service. You can also have Petitions from the members freely given the advice on how to do it. You can also advise members of the public to move Statements and Motions through you for purposes of being processed by the Assembly.

#### CONDUCTING BUSINESS WITHIN COVID-19 GUIDELINES

You would recall that the Covid-19 pandemic was reported in Kenya in March of last year and really it has changed the way we conduct our business. The World Health Organization (WHO) and our Ministry of Health (MOH) have been issuing public health protocols on how to conduct business in the public so that we cut the spread of the pandemic.

We have been advised to continue washing of hands frequently and I am happy to have seen the Hon. Members doing that here and guiding members of the public. Sanitizing and screening of temperature to be allowed within this area. We are also wearing masks and I am

sure that every Hon. Member has led by example and I can see the public in the gallery are also wearing face masks.

We also keep social distance of at least 1.5 meters so that we are able to remain safe. So keep to your seat Hon. Members and also members of the public in the gallery so that we do not change chairs; the one you have been using keep using that one until we finalize and the Serjeant-At-Arms and the law enforcement officers will assist you in following these guidelines. Thank you, Hon. Members.

**STATEMENT SOUGHT**  
STATUS OF IMPLEMENTATION OF TENDERING  
METHOD TO GRADE COUNTY ROADS

**Hon. Speaker:** Hon. Members, under this Order, we have one business by the Hon. Eric Musembi.

**Hon. Musembi:** Thank you, Madam Speaker.

Hon. Speaker, the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya, 2010 mandates County Governments with County transport including county roads;

Hon. Speaker, the County Government of Machakos through the Department of Transport, Roads and Public Works has been grading feeder roads using County equipment and plants that in most cases are not convenient because of breakdown and lack of adequate fuel;

Hon. Speaker, it is worth noting that the County graders are shared one per Sub-County whereby Machakos Sub-County has one meant to serve seven Wards;

Hon. Speaker, Kola Ward to be specific has not been served by the grader for the last two years;

Hon. Speaker, a motion to adopt tendering method to grade County roads from the FY 2019/2020 was moved and approved by this Hon. House on 14<sup>th</sup> May, 2019 during *Bunge Mashinani* at Ndithini Ward;

Hon. Speaker, pursuant to Standing Order 41(2), I wish to seek Statement on status of implementation of the said motion that resolved that the House discusses and approves that the County Government of Machakos:

- i. Adopts tendering method to grade county roads from the FY 2019/2020 on wards.
- ii. Repairs all graders and station them at the Sub-County offices whereby they can be utilized to undertake emergency works road and minor repairs within the sub-counties.

Thank you, Madam Speaker.

**Hon. Speaker:** Thank you Hon. Eric Musembi. Hon. Members, as it is the tradition this being a Statement, perhaps we could have a few comments from any member so that we can agree on the way forward. Hon. Museku.

**Hon. Museku:** Thank you, Madam Speaker. I would like to thank Hon. Eric for the Statement which he has brought here today concerning the issue of graders and grading of our roads. Madam Speaker, it is common knowledge to all of us here Hon. Members, our roads are in a pathetic state. We know that for the last two years right now the grading programme which

is being undertaken by the county government has not been working properly due to various reasons including poor maintenance of the equipment which we have which are the graders and also for us here in Machakos Town sub-county because my ward in Machakos Town sub-county, when we have one grader to serve seven wards, you will find that if you go to an area like Mavoko, they only have four wards and they are given a grader.

Machakos sub-county has seven wards and we are given one grader so by the time the grader comes to your ward, it has taken a very long time and very many breakages are happening. Madam Speaker, that is the reason why the Statement brought by the Hon. Member for this area is very pertinent. Because of the many roads which we have, it is not possible for the county government to effectively grade all the roads in the wards using their equipment and that is the reason we sought to get contractors to be able to assist the county government graders in doing this work. If we could be able to engage contractors it will ensure that at least every ward every year is graded twice.

In our budget,s, Madam Speaker, we normally put a budget of grading 45km per ward and we allocate the money there; in the current year financial budget 2021/2022, we have allocated Ksh. 90 million for maintenance and over Ksh. 80 million for fuel of our graders. So, with Ksh. 90 million for maintenance of the equipment and over Ksh. 80 million of fueling the graders, Madam Speaker, there should be no reason whatsoever why we should not be able to do as much grading as possible. In addition to that, we have allocated about Ksh. 240 million to contracting of rural roads through Kenya Roads Board (KRB) and other contractors.

So, Madam Speaker, I think that motion which was moved before the House or approved by the House for the county government to ensure that they contract and also maintain their equipment and for those wards, for those sub-counties like Machakos Town sub-county get additional equipment; have at least two graders in those sub-counties with many wards and that will be able to assist this county very much and assist our people because they are suffering. Actually, Madam Speaker if I may just tell you some of the Statements, I hear like people saying and I quote; *twisilaa masyukoni* (We travel on rugged roads)

**Hon. Speaker:** Point of order Hon. Museku, you will pick it up from that. Hon. Ndawa what is the point of order?

### PROCEDURAL MOTION EXTENSION OF SITTING TIME

**Hon. Ndawa:** Thank you, Madam Speaker. I am raising on Standing Order 27; Madam Speaker, the morning session is supposed to end by 12.30 Pp.m. and looking at the business ahead of us and whatever is contained in the Order Paper, I am requesting that we pass the motion to adjust time so that we can be able to transact all the business which is in the Order Paper.

**Hon. Speaker:** Mr. Dominic here, can I have the question to propose for extension of time. Thank you, Hon. Ndawa. Alright I hear you. Hon. Members, even as we seek to extend the time, under Standing Order 27, *tukumbuke kwamba tuko mashinani na tukiongea tunaweza kujaribu tuongee Kiswahili. Tunaruhusu, tutakubaliana turuhusu kuchanganya, lakini tukichanganya kiswahili kiwe ndio kiko sehemu kubwa ya kuongea kwetu ndio tuweze kusikizana hapa Bunge mashinani.* Hon. Ndawa, do you have a seconder to your motion to extend sitting time?

**Hon. Ndawa:** Thank you, Madam Speaker. I call upon Hon. Moffat Maitha to second my motion.

**Hon. Speaker:** Thank you. Hon. Moffat Maitha.

**Hon. Maitha:** Thank you, Madam Speaker. I support that we extend time. Thank you.

*(Question proposed)*

**Hon. Speaker:** Can we have comments on that proposed question. Any Member who is opposed to that proposal?

*(Question put and agreed to)*

You can proceed, Hon. Museku.

*(The House resumed business as per the Order Paper)*

**Hon. Museku:** Ahsante sana, Madam Speaker. Kwa hivyo kama vile nilikuwa nasema nikwamba watu wetu kule nyumbani sasa barabara zimeharibika, watu wanasema; twisilaa masyukoni, inywi mwisilaa lamini nundu mwina ngali, naitu twisilaa masyukoni. Na kama waheshimiwa tukisikia watu wetu wakisema wanapitia kwa masyuko hiyo kitu inatuguzua sana. Kwa hivyo, tunauliza serikali huyo mjadala ambao uliletwa kwa bunge na Bunge ikaamua kwamba *County government* ya Machakos ifanye vitu mbili; *ienagage contractors* maanake zile *grader* ambazo wako nazo haziwezi tosheleza kufanya kazi Kaunti nzima.

Kwa hivyo wa *engage contractors* mahali ambao wanaweza ku *engage contractors* na pia wa *maintain* hizo *graders* mwaka huu tumewawekea pesa nyingi sana. Tumewawekea milioni tisini za *maintenance of the equipment*, tukawawekea milioni themanini ya mafuta na kwa *equipment*. Pia tumeweka zaidi ya milioni 240 ya *contracting* ya barabara. Kwa hivo, tunahimiza kama vile Mheshimiwa ameulizia ni vizuri *county government* ifuatilie hizo vitu zifanyike na sub-county zile ambazo ziko na wodi nyingi kama hii yetu ya Machakos Town ambao tuko na wodi saba, *grader* ilifanya kwangu mwisho 2019 September na mpaka sasa haijawahi kamilisha kwenda *round ward* zote saba and *we are talking about* miaka mbili *down the line*.

Kwa hivo naunga mkono hiyo *Statement* Mheshimiwa ameleta na tunaomba kwamba serikali ifuatiliehiyo maneno. Asante sana *Madam Speaker*.

**Hon. Speaker:** Shukrani Mheshimiwa Museku. Nitapatia nafasi waheshimiwa wale wako na mikono juu. Mheshimiwa Hellen na tuongee kwa haraka kwasababu tuko na mambo mingi bado tunafaa kufanya.

**Hon. (Ms.) Ndeti:** Asante, *Madam Speaker*. Nasema asante kwa Mheshimiwa wa hapa ambaye ni Mheshimiwa Eric Musembi. Hii *Statement* ameleta *is very timely* kwasababu vile nimeona serikali yetu tangu iundwe haijawahi kutenga pesa kiasi *enough* ya

kununua *machines* ambazo ni mpya na ambazo hazitakuwa *zinabreak* wakati kazi ianendelea. Kwa hivyo yangu nikuuliza hii serikali yetu *this is our last budget* lakini sasa tukienda *next budget* tuongezee pesa ndio wanunue *machines* za kutosha vile kaunti zingine zimewfanya. Kila *ward* iwe na *machine* mbili au tatu ndio njia zote zitengenezwe. Hapo ndio naona tumewenda kombo kidogo lakini najua tukiendelea hivo, hizo pesa zitatengwa na njia zetu zitatengenezwa.

Lile ingine nimeunga mkono pia ni mahali amesema tuanze kufanya *tendering because* hizo *machine* hazitoshi kwa sasa. Kila mtu anataka apitie njia ambayo ni nzuri. Hata wale wako na *motorbikes* hata kama sio gari tunataka njia ambayo wateja wako hawaanguki kwasababu hiyo ni mbaya. Kwa hivyo ni vizuri tuanze ku *tender* tuchukue watu ambao wanaweza kuja watusaidie kujenga manjia zetu. Asanteni.

**Hon. Speaker:** Asante Mhehsimiwa Helen Ndeti. Mheshimiwa Nyanzi.

**Hon. Nyanzi:** Asante, Spika. Nataka kupongeza Mheshimiwa wa hapa kwa kuleta hiyo mswaada ili mabarabara yetu iweze kutengenezwa kaunti yote. Na kwa vile mimi nimetoka hapa, taabu ambayo tuko nayo ya barabara hapa Kalama ni kubwa sana sababu hizo ward saba zimesemwa, Kalama na Kola tuko ndani, tumeunganishwa na Machakos Town ambayo ni town imekuwa na bahati kwasababu sehemu nyingi ni mlima.

Hapa Kalama ni kubwa sana; ni mara karibu tatu ya Machakos Town yote. Kwa hivyo naomba ikiwa hizo tingatinga zitanunuliwa, zinunuliwe na Kalama ipewe tingatinga yake peke yake sababu area yake ni kubwa sana ili iweze kutengenezwa. Asante sana.

*(Applause)*

**Hon. Speaker:** Asante, Mheshimiwa Nyanzi. Mheshimiwa Ndawa halafu Mheshimiwa Maitha.

**Hon. Ndawa:** Thank you, Madam Speaker. *Naomba kwa heshima---*

**Hon. Speaker:** Na tujaribu tuseme kwa ufupi.

**Hon. Ndawa:** Thank you, Madam Speaker. *Nataka kwanza nishukuru wakaazi wa Kola ward kwa kutuletea Mheshimiwa ambaye amejitolea kwa kazi yake. Najua walikuwa wengi wamesimama lakini mliangalia mkaona huyu ndiye anaweza. Nataka niwaambie nyinyi ni werevu na mlileta the right person.*

Secondly, Madam Speaker, *nataka nimshukuru Mheshimiwa kwa hiyo Statement ambayo ameuliza ya mambo ya barabara. Madam Speaker, kama vile tujuavyo sisi zote tulikuwa kwa Bunge ambayo ilikuwa pale Ndithini na mswaada uliletwa na tukapitisha; sasa Madam Speaker, ile kitu naulizia ni mwenyekiti wa kamati ya Implementation pamoja nba hiyo kamati ya Implementation, sababu sheria inasema motion ikipitishwa kwa Bunge inakuwa committed kwa hiyo committee ya implementation.*

Madam Speaker, *sitaona haya nikisema ya kwamba hiyo Committee ni kama imelala kwa kazi yake kwa sababu haijawai leta ripoti tena kwa Bunge ikatuambia tumefika mahali fulani, sasa hiyo Statement imekuja so nataka niwaambie wajikaze na wafanye kazi yao. Tukiona*

hiyo committee haifanyi kazi, tunaweza vunja hiyo kamati na tupatie watu ambao wako tayari kufanya kazi.

*Ile kitu ingine ningesema Madam Speaker, kazi ya Bunge inajulikana, na kazi ya barabara inajulikana ni kina nani wanafaa kutengeneza barabara. Barabara ikiwa na mabonde, mabonde wakaazi wa hapa wataanza kupiga Mheshimiwa wa hapa kusema hajakata barabara, na ni vizuri tuwaambie wakaazi wa hapa ya kwamba kazi ya kukata barabara sio kazi ya Mheshimiwa. Kazi ya Mheshimiwa ni kutunga sheria na wengine wanafanya hiyo kazi. So, kama barabara ni mbaya hapa, tafadhali msianze kushurutisha Mheshimiwa kwa kazi ambayo sio yake; ile yake anafanya na anafanya kwa haki, na hajawahi chelewa kuwakilisha nyinyi kwa bunge.*

Madam Speaker, *lile jambo ingine ningekuwa nalo ambayo inaonekana kama iko kando kidogo, wakati Rais mstaafu wa Amerika aliingia hapa kenya, kuna jambo alisema. Alisema we are living in a world of limited resources. Mahitaji ni mengi lakini vitu ya kufanya hiyo mahitaji hatuna kabisa. So, Madam Speaker, ijapokuwa tumepitisha motion ya kwamba kazi zite zipewe contractor ama ziwe contacted. Madam Speaker, kulease that machine or grader for one hour---*

**Hon. Speaker:** Hon. Ndawa, you are getting out of order, you are out of order. Can you stick to the motion on the table? If you want to challenge the motion you passed as an Assembly, bring another motion. *Kwa hivyo sasa endelea na kile tulikuwa nacho kwa meza.*

**Hon. Ndawa:** Well-guided, Madam Speaker. But my proposal was as we sought or as we look for ways of contracting, let us have the current graders serviced, let them have fuel and let them go and grade our roads. Madam Speaker, I tend to wonder, how come that the county graders are breaking down and the contractor graders are not breaking down. You give a road to a certain contractor he is going to do that road for almost one month without breakage but the county grader the moment it reaches your ward, two hours it is broken down.

So, Madam Speaker, I strongly believe that these things are broken down deliberately. Somebody somewhere is trying to sabotage; he is trying to betray that the MCAs are not doing their work. Right now, we are in Kola ward, doing what we were elected to do and we are going to do it in the right way. So, Madam Speaker, I support the Statement and I request that you give direction that we get a response within the shortest time possible. Thank you, very much, Madam Speaker.

*(Applause)*

**Hon. Speaker:** Thank you. Asante Hon. Ndawa; Hon. Maitha. *Nawakumbusha waheshimiwa tujaribu kufupisha misemo hii ni Statement tu, sio Motion.*

**Hon. Maitha:** Thank you, Madam Speaker. Madam Speaker, *niseme ya kwamba naunga mkono hii Statement kutoka kwa Mheshimiwa musembi, nikisema ya kwamba vile Mheshimiwa Ndawa amesema, kazi ya Mheshimiwa Mbunge wa County Assembly, ni kutunga sheria, kuangalia vile Gavana na serikali inafaya kazi lakini kazi ya barabara ni kazi ya serikali na wananchi wakiona barabara zote zimekuwa mbaya, waamuke na waambie serikali kazi haifanyiki.*

**Hon. Speaker:** Mheshimiwa Maitha waelewa kwamba wewe pia ni serikali? Unafaa kuongea ni serikali gani; wewe ni serikali, kama Mbunge wewe ni serikali.

**Hon. Maitha:** Serikali yaani *the county government executive*, ile *county government* ya Gavana Mutua, tuseme barabara zimeharibika vibaya sana. Ukienda kule Matungulu West---

*(Loud consultations)*

**Hon. Speaker:** Order, Hon. Members.

**Hon. Maitha:** I don't want to be taught by anybody here; I became a politician long time ago.

*(Laughter)*

**Hon. Speaker:** Hon. Maitha, stick to the agenda. *Ongea juu ya kile kiko kwa meza.* Hon. Maitha, proceed.

*(Loud consultations)*

**Hon. Maitha:** Kule Matungulu West nina 11 *sub-locations* na kutoka one *sub-location* kwenda kwa ile ingine zote 11, inachukua muda na vile Mheshimiwa amesema hizo *graders* zinaharibika na ikiharibika saa zingine inakubidi wewe Mheshimiwa utengeneze *the part which is broken.* Tyres zikitoboka na *puncture* saa zingine ni wewe unatumia pesa zako utengeneze hizo *tyres.* Kile ningomba serikali yetu ya *county government* na *the executive* ni kwamba pesa tukiwapatia, *let there be equity in the usage of that money to all sub-counties and the whole wards.* Si pesa zikionekana *ward* moja iwe na barabara zile nyingi za lami zingine kama kwetu hakuna lami inaonekana. *Please can you give me time.*

**Hon. Speaker:** Hon. Maitha.

**Hon. Maitha:** Thank you, Madam Speaker.

**Hon. Speaker:** Thank you Hon. Maitha, Hon. Members, the Statement, as you have commented is committed to the Implementation Committee and the committee should report to this House by 7th July, 2021, that is 14 days.

*(Applause)*

## MOTIONS

### DESILTATION OF DAMS AND RETICULATION WATER IN KOLA WARD

**Hon. Speaker:** Hon. Members, under this Order, we have one business by Hon. Eric Musembi.



*(Loud consultations)*

Hon. Ndawa, can we have order in the House.

**Hon. Musembi:** Thank you, Madam Speaker.

Hon. Speaker, that aware that Article 174(f) of the Constitution of Kenya, 2010 stipulates that one of the objects of devolution is to promote social and economic development and the provision of proximate, easily accessible services throughout Kenya;

Aware that the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya, 2010 bestows the County Government with matters of implementation of specific national resources and environmental conservation, including soil and water conservation and water and sanitation Services;

Hon. Speaker, further aware that the mission of the water and irrigation sector according to the County's ADP for the FY 2020/2021 is to contribute to county development by promoting and supporting water resource management to enhance safe water availability and accessibility for all;

Hon. Speaker, acknowledging that the residents of Kola Ward and the larger Kalama Sub-county source water from earth dams specifically Lumbwa, KyakatoIwe and Kola dams

Aware that most of the boreholes previously drilled by the County Government of Machakos in the Ward were not productive hence dry. This is a clear indication of a low water table;

Aware that the existing dams, if well de-silted, can hold greater volumes of water and serve a wider population;

Further aware that water from these dams can be reticulated and distributed in the growing markets, homesteads and farms for use;

Hon. Speaker, I wish to move the motion that this Hon. House discusses and approves that the County Government of Machakos;

1. De-silts all the existing dams in Kola and the larger Kalama sub-county.
2. Reticulates water from all the existing dams for the benefit of the residents of the Ward.

Thank you, Madam Speaker.

**Hon. Speaker:** Kwa kifupi, Mheshimiwa Eric unaweza kuelezea Bunge kwa faida ya wananchi ambao wako kwa *gallery* mswaada wako ni juu ya nini kwa Kiswahili.

**Hon. Musembi:** Kwa wananchi wa Kola, nawasalimia. Kwa kwa hoja ambayo tuko nayo ni maneno ya maji (.....Inaudible) tujadiliane tujue vile tutasaidia watu wetu wa Kola na Kalama. Asanteni.

**Hon. Speaker:** Asante sana Mheshimiwa Eric. Nani anakushika mkono kwa hii hoja?

**Hon. Musembi:** I call upon Mheshimiwa Nyanzi *to second*.

**Hon. Speaker:** Mheshimiwa Nyanzi, umeulizwa ushike mkono hii hoja.

**Hon. Nyanzi:** Kwa Spika, nasimama hapa ku *second this motion*.

**Hon. Speaker:** Asante Mheshimiwa Nyanzi.

(Applause)

Hon. Members, *kwa sababu swala limetengenezwa kwa Kimombo nitasoma kwa Kimombo.*

(Question proposed)

Hon. Members, the motion is open for debate. Hon. Mitaa.

**Hon. Mitaa:** Asante, Bi. Spika kwa wakati umeniruhusu nichangie hiyo hoja ya Mheshimiwa Musembi. Bi. Spika, huu msawa ni wa manufaa sio tu kwa wakaazi wa kalama au Kola, lakini Machakos yote. Bi. Spika, mabwawa yanauwezo wa kuweka maji ya kiwango ya juu na mabwawa yakitunzwa vizuri maji yake yatatumika mwaka wote.

Bi. Spika, kama mabwawa yako na maji, matumizi yake ni mengikwa maana hayo maji yanaweza kutumika kwa matumizi ya nyumbani, hayo maji yataweza kutumika kwa matumizi ya kunyunyizia mashamba yetu tupate chakula, hiyo maji yataweza kutumika kwa mifugo, kwa hivyo ile jambo mimi naweza uliza kaunti ya Machakos kupitia kwa kilre kitengo cha *Executive*, ni kuwauliza ama kuwahimiza waweza kuweka pesa mingi ndio zile bwawa zote ziko katika hii eneo ya Machakos ziweze kuangaliwa, wanunue zile mashini zinaweza kutoa hiyo mchanga hata watafute pesa ya kusafisha yale maji ndio yatoke kile kiwango cha uchafu yaweze kutumika kwa mambo kama ya upishi na maneno ya kufua manguo kwa manyumba ndio wananchi wa Machakos wafikie kunufaika kutokana na hayo mabwawa kwa maana eneo letu lina uwezo na tuko na mito mingi ile tunaweza kutumia kupata hayo maji hasa wakati wa mvua, ndio saa za kiangazi zikifika, yale maji yafikie kutumiwa na wananchi wa machakos.

Kwa hivyo naunga mkono huo msawa wa Mheshimiwa Eric Musembi na nimshukuru kwa kufikiria katika jambo lile wananchi wa Machakos wanaweza saidika. Asante.

**Hon. Speaker:** Shukrani Mheshimiwa Mitaa. Mheshimiwa Dominic. Nitawapatia nafasi Waheshimiwa.

**Hon. Ndambuki:** Asante, *Madam Speaker*. Ningependa kumpongeza Mheshimiwa Eric kwa mjadala ambao uymeleta leo Bungeni tuongelelee mambo ya kusambaza maji kwa eneo la kalama na kola. *Madam Speaker*, pia nikingeze ingekuwa ni heri pia kama *Executive* kando na kusambaza maji ya mabwawa, ingetengeneza *treatment plant* ili haya maji ambayo tutakuwa tumetega pale kwa mabwawa yaweze kutumika nyumbani, watu waweze kuyatumia kupikia na pia kunywa.

*Madam Speaker*, pia eneo hilila Kalama linma mashamba mengi makubwa; haya maji tukiyatega vizuri yanaweza kutumika kwa upanzi wa chakula na watu wa hapa wanaweza kujikuza ki uchumi. Asante Bi. Spika.

**Hon. Speaker:** Asante, Mheshimiwa Dominic. Mheshimiwa Rozina.

**Hon. (Ms.) Rozina:** Thank you, Madam Speaker. Madam Speaker, *mimi ni mkaazi wa Kalama kwa hivyo nikiwa hapa niko nyumbani. Asante sana Mheshimiwa Eric kwa hiyo motion. Na mimi nikiwa mkaazi wa Kalama na wewe ukiwa mkaazi wa Kola tutasaidiana kwa hiyo motion. Madam Speaker, wakati wa by-elections za useneta ambayo imeisha, mimi nilikuwa na bahati ya kutembea Kalama na Kola na naweza attest hii motion Mheshimiwa ameleta hapa ni ya ukweli.*

*Hizi area mbili ziko na uhaba wa maji kwa hivyo nitashikana na Mheshimiwa Eric na Mheshimiwa Paul Nyanzi tusukume hiyo na mimi nikiwa katika Implementation committee nitahakikishia watu wa hapa hiyo motion itaenda through. Asante sana.*

**Hon. Speaker:** Asante sana Mheshimiwa Rozina. Mheshimiwa Kisini.

**Hon. Kisini:** Asante sana, *Madam Speaker*. Nataka kusema kwanza Mheshimiwa Eric ni asante kwa kuleta hiyo *motion* ya kuangalia mambo ya maji, hasa maji ya hapa Kalama. Nataka kusema ya kwamba hiyo motion ambalo imeletwa na Mheshimiwa Eric ni nzuri sana sababu itasaidia eneo lote la kaunti ya Machakos. Mimi ndiye *chairman wa environment, lands and natural resources* na upande wa maji iko katika hiyo *department*. Nataka kusema ya kwamba kuna *motion* ambayo ilikuja ya kwamba tufanye hiyo *de-silting*, tutembe kwa *dams* zote katika eneo lote an tulifanya hivyo na tulitoa *report*.

Yaani nataka kusema ya kwamba tulitembea kwa masilanga yote ya kaunti ya Machakos, na tukatoa ripoti na hata tukasema hizo silanga zote ziangaliwe na uchafu yote itolewe na uchafu ikitolewa hiyo maji ipigwe au hiyo *reticulation* isambazwe kwa wananchi. *So*, nataka kusema ya kwamba hii *motion* leo imeletwa na Eric *it was timely*, ukitaka watu wa kola wasaidike hata sisi tunaomba watu wa Machakos wote wasidike kupitia kwa hiyo *motion* yako na hasa watu wa Athi River ambao tunajua ni *town* na pia hawana maji. Asante sana, Bi. Spika.

**Hon. Speaker:** Asante Mheshimiwa Kisini. Mheshimiwa Nziva.

**Hon. (Ms.) Nziva:** Asante Bi, Spika. Napenda kuunga mkono na kushukuru Mheshimiwa Eric kwa kuleta hii mjadala. Hakika maji ni uhai; watu wa Kola hata Kalama watasaidika sana na maji. Wakati tunachimbua hizi bwawa hakika watu watasaidika sana haswa tukireticate ama tuki sambaza hiyo maji kwa maboma mbali mbali, watu wa Kola na Kalama watasaidika sana, hata *even the reticulation* tukifanya *treatment* watu pia watumia maji safi, watanywesha mifugo yao, pia hata *economy* ya hiyo *area* itainuka sana kwasababu nakumbuka *area* nyingi ziko na maji, hakika hata watu wamejenga nyumba mzuri, wamejenga sawa sawa na uchumi imakuanga imepanda sana.

Kwa hivyo nasema Mheshimiwa asante sana kwa kushughulikia watu wako wenye walikuchagua na hakika Mungu atakusaidia sana na *county government* tukifanya *even in the other wards* watu watapata maji na watajiendeleza maishani mwao. Asante sana Bi. Spika.

**Hon. Speaker:** Asante, Mheshimiwa Nziva. Mheshimiwa Musyimi.

**Hon. Musyimi:** Asante sana, Bi. Spika. Bi. Spika nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Eric ambaye ni wa hapa kwa kuleta huo mswaada ambao unachangia kuhusu maji. Mheshimiwa mambo ya maji kusema kweli vile hata wengine wamesema, maji ni uhai, pasipo na maji kuishi ni vigumu. Bi. Spika nasema huu mswaada umeletwa wakati unaofaa; wakati ambao tuko nikifikiria ile msimu miwili ya mvua uliopita hakukunyensha vizuri na sasa ndio wakati mzuri wa kutoa hiyo mchanga ambao umefunika bwawa zetu za maji maana ni wakati ambao hizo bwawa hazina maji mingi.

Kwa hivyo Bi. Spika kama serikali ingeamua kutoa huo mchanga wakati huu, hii ndio wakati mzuri maana hata hakuna maji mingi itaaribika maana hizo bwawa ile maji ikop huko ni kidogo tukiingoa ule msimu tunatarajia kuja ambao ni mwezi wa kumi ndio tunatarajia ile mvua ambayo tunatarajia inaweza kuja na maji mingi.

Kwa hivyo Bi. Spika, huu ndio wakati ambao unafaa hiyo mchanga itolewe kwa mabwawa na nikiuliza ingekuwa ni vizuri huo mswaada ungetakuwa unataja Machakos yote mahali kwote ambao kuna bwawa maana tukiongelea pande moja kwingine kutazama. Bi. Spika, mimi nitafikahapo na ninasema ni Asante hiyo ni mswaada ambao unafaa. Asante sana.

**Hon. Speaker:** Asante Mheshimiwa Nzomo. Mheshimiwa Johana; nitawapatia nafasi waheshimiwa.

**Hon. Munyao:** Asante Bi. Spika. Bi. Spika, mambo ambayo tukiangalia kutokana na Katiba ya 2010, mambo ambayo yaliteremshwa kutoka serikali kuu kuingia kwa serikali za kaunti, wenye walikuwa wanatenganisha mambo ambayo yatabaki kwa serikali kuu na mambo yenye yataiteremshwa kwa serikali za kaunti, ukiangalia vizuri utakuta ya kwamba mambo yenye yaliteremshwa ni mambo ambayo yanaguzwa maisha ya mwananchi. Ya kwanza ni maji, ya pili ni barabara zenye tumeogelelea muda mfupi uliopita ambazo ni za huko ndani mashinani, mambo kama kilimo ambao tunakuza chakula. Kwa ufupi ni mambo ambayo ni yale *basic* kwa mwananchi.

Lakini nazo pesa ambazo zinankuja mashinani ni pesa haba kidogo. Nikiunga mkono mjadala ambao umeletwa mbele ya hii Bunge na Mheshimiwa wa hapa Kola Mheshimiwa Eric, ni kwamba ni vizuri kukubali ya kwamba hii sehemu ya Kalama *sub-county* ni sehemu ambayo iko na mashamba makubwa, ni sehemu hata tukiangalia wakati huu ambao sio msimu wa mvua, utaona ni kama imeanza kukaa kama ni jangwa kidogo.

Ningesema ni vizuri wakati watu wanafanya utafiti tunaelewa ya kwamba kuna sehemu za hii Machakos County ambazo zinaweza fanya vizuri kwa mambo ya *boreholes* na sehemu zingine zinaweza fanya vizuri kwa mambo ya mabwawa na tuhakikishe ya kwamba tukiweka raslimali kuhakikisha ya kwamba tume faidi wananchi, tunatenda yale ambao yanapaswa kwa shehemu kwenda sehemu ile nyingine. Kuna mambo ambayo yanaweza fanya vizuri kwa sehemu fulani kinyume na vile hao mambo yanaweza fanyika kwa sehemu zingine.

Hii Kola *ward*, kwangu naona mambo ya mabwawa ni mambo ambayo yanapaswa kupewa kipao mbele ili tuhakikishe ya kwamba tumepanua yale mabwawa yako katika hii sehemu halafu maji yasafishwe na yawe yamesambazwa kwa wananchi. Kwa hivyo Eric Mheshimiwa huu mjadala umekuwa kwa wakati unaofaa na tunaomba tutaendelea kukusaidia ili tuhakikishe yakwamba wananchi wa Kola, na Kalama *sub-county* kwa jumla wamesaidika. Asante sana Bi. Spika, kwa kunipea hiyo nafasi.

**Hon. Speaker:** Asante Mheshimiwa Johana. Mheshimiwa Alice. *I will come to you Members; remember we also have other businesses.*

**Hon. (Ms.) Nzioka:** Asante, Bi. Spika. Bi. Spika nichukue fursa hii kukushukuru ni kwa ajili ya Bunge mashinani. Bunge lililopita la mwaka wa 2013 nilikuwepo mpaka 2017 nanikajaliwa tena kurudi katika bunge. Umeleta bunge mashininani ili kila mwananchi ajue, kwa sababu ukiangalia kama sehemu ya Kola mtu kutoka hapa kuja Machakos ni kwa ajili ya kuona vile bunge linanafanya kazi, itakuwa ni vigumu, lakini kwa mipango yako ukatengeza tuwe tukija mashinani ili wananchi wajue viongozi walio wachagua, pia walioteuliwa na vyama jinzi ambavyo wanawawakilisha katika bunge la Machakos.

Ni sehemu moja mimi nimeona kama Mheshimiwa katika bunge ya Machakos. Ni sehemu moja mimi nimeona kama mheshimiwa katika bunge ya Machakos umefanya kazi nzuri, na ni kazi ambayo mtu akiangaliwa akifanya kazi nzuri kama ingewezekana ningekupa zawadi sababu umefanya kazi nzuri.

Pili kongole mheshimiwa Eric tumekaribishwa kwako tumekuja na nimesikiza vile ambavyo ulianza. Mambo ambayo ni ya Mheshimiwa katika bunge la Machakos ni mambo matatu; kwanza ni kutunga sheria, na wakati ambapo tunatengeza sheria bungeni huwa uko bungeni ili kusikiza watu wa Kola watapelekwa aje. Pili umewawaakilisha kuleta mashida yao kama vile leo umesema kwamba barabara katika wodi ya Kola, maji haipatikani juu ni sehemu ya milima milima.

Tatu kazi ya ambayo inatendeka kama hii kazi itanza, ni jukumu yako kama mheshimiwa kuangalia kwamba, kama zile pesa zimewekwa kwa mradi zimefanyiwa kazi nzuri. Mimi ningependa kusema kamati tekelezi ambayo tunayo katika bunge letu, sasa hii imeletwa mara ya pili, tulikuwa na bunge mashinani sehemu ya Ndithini na tukasema kwamba, barabara zote maana vyombo ama vyombo ambavyo vinatengeza barabara za County zimeleta shida. Mara tingatinga imeenda imevunjika, mara sijui nini, ni kama kuna mpango ambao sio mzuri katika County.

Tukasema kandarasi zipeanwe, ili barabara zitengenezwe. Kamati tekelezi tafadhali, kama mambo imeshindikana mrudi katika bunge mtuambie mambo imeshindikana, sisi kama bunge tunauwezo wa kufuatilia katika serikali ambayo inaongozwa na Gavana Mutua tujue, na mimi najua Gavana wetu ana nia nzuri ni kwa ajili ya maendeleo katika County. Lakini kuna wengine hapo wana mipango na tunataka kujua.

Mheshimiwa Eric nataka ujue huu msawa ambao umeleta, maji ni uhai na sehemu hii itakuwa ngumu sana watu wa hapa kuwa na maisha mazuri bila maji. Hayo mabwawa ambayo umesema yafukuliwe yote maana County inaweza na ina huo uwezo. Na watu wa Kola watakaa vizuri maana walikupa huo uwezo. Kuchaguliwa unaletwa bunge kwa sababu una huo uwezo. Kwa hivyo najua sisi kama bunge tutashikana pamoja ili tukuunge mkono mambo yawe mazuri.

Mwisho wananchi wa Kola, mimi nawashukuru. Unajua watu wanachagua kiongozi na *maybe* hawatajua wamechagua nani. Watu wa Kola walichagua mheshimiwa Eric na ni mheshimiwa ambaye hana mambo mengi lakini wakati anasimama na kuongea unaskia kweli alichooongea amekipanga na ni kwa ajili ya watu wa Kola. Kwa hivyo nawashukuru na vile mmekuja Mungu awabariki, Bi Spika, Mungu akubariki na wakati ambapo unafanya mazuri, Mwenyezi Mungu anakulipa. Naomba hio kazi nzuri unaendelea kutenda Mwenyezi Mungu

akulipe na najua nita nitafurahi wakati mmoja, nikisema Mungu amekulipa. Asante sana, *thank you very much.*

**Hon. Speaker:** Asante Mheshimiwa Alice. Mheshimiwa Kingo'ri alafu Mheshimiwa Kituku; nitakuja tu Waheshimiwa, nitakuja, *I will come to you.* Mheshimiwa King'ori alafu Mheshimiwa Kituku. Na tujaribu kufupisha tafadhali.

**Hon. King'ori:** Asante Bi. Speaker, yangu itakuwa machache tu. Isipokuwa kama ningepewa nafasi katika kifungu ya Standing Order 50 ambayo inatukubalia kufanya marekebisho kidogo katika msawa wakati unaendelea, tubadilishe tuseme, badala ya kuwa, iwe ni Kola na Kalama, iwe ni katika County nzima sababu tumeshaweka pesa katika *environment* ambayo inakuja, na hii inataka niongeleshe wakaazi wa hapa. Najua kuna *Bill* tulipitisha ya *Environment* ambayo pia tunatarajia mwezi wa tisa, italeta Ksh. 1.2 B ambayo itashugulikia maneno ya maji na inaegemea upande wa *environment* peke yake.

Katika ile *Bill* yetu *Madam Speaker*, ya *Climate Change Bill*, ambayo saa hii ni *Act*, ambayo imeanza kutekelezwa. Ile kitu ningeomba, kwa sababu pia kuna *Committee* ambayo imechaguliwa hapa Kola, wa hio *committee*, waangalie ile miradi mzuri ambayo zinahusu nyinyi wananchi ndio mpatiane wakati mtakapokua mnajadiliana maneno ya hio *Bill*, sababu hio pesa ni mingi ambayo itakuja kila ward kwa hivyo hio jukumu mumepeva nyinyi na Katiba kushugulikia ile kazi itafanywa kwa kila ward na pia tukaona kwa hio *Bill* tupatie nyinyi nguvu ya kufanya kazi ile mnataka nyinyi wenyewe.

Alafu ndio mwakilishi wenu ambaye yuko hapa na anafanya kazi mzuri, awe na kazi ya kufanya bungeni kuuliza ile kazi wananchi wangu walipatiana mlifinya? Hio ndio ile kitu ambayo Bi. Spika ningetaka kunena kidogo.

Alafu niseme namna hii; hii pia maneno ya maji, ni kitu ya muhimu katika *County* mzima na sasa ni wakati mzuri tuhakikishe ya kwamba hii kazi inafanyika katika njia ile inayofaa. Kama ni *Department* fulani imekataa kufanya kazi tuiseme ukweli, lakini tukisema maneno ni *County Government*, ndio ni *County Government* ambayo mimi ni mwenye serikali hio, lakini mimi nafanya katika kiwango gani? Ni lazima pia niambie wananchi kiwango kile siwezi vuka kwasababu kipengee 174(g) ya katiba ya Kenya inatukataza kufanya kazi ya Governor inatuambia tuangalie separation of powers. (??).

Kifungu ya 175 pia inarudia, ndio ya kwanza, inahimiza *separation of powers* na ndio katika ile *Bill* Bi. Spika, hatukuweka mahali at MCA, atasimamia miradi ya hio *Bill* kwa sababu katiba imetukataza kufanya kazi mbili. Kwa hivyo mwananchi ni lazima ajue ni nani hajafanya kazi na ni nani amefanya kazi ndio tusikuwe na vita tukisemekana kuwa MCA anafaa kufanya, wengine wamepotosha wananchi wakisema MCA anafaa ajenge barabara ama afuate Governor ama aende kwa Governor afanye kitu. Hiyo yote hatufanyi; tunafikisha kwa bunge, juu wakati tunapatiana *budget* hakuna mtu anaweza simama peke yake apinge bunge.

Kwa hivyo hii kitu ni ya ushirikiano ya bunge yote ambayo inaongozwa na Bi. Florence Mwangangi, ambaye kazi yake anafanya kama wakili ambaye anaelewa sheria. Kwa hivyo *Madam Speaker* na kucongratulate wakati unafanya kazi huna mapendeleo, na hio ni kitu ya muhimu katika hii county. *Thank you, Madam Speaker.* Majina yangu ni George Kariuki Kingori na nimechaguliwa Muthwani sio *nominated*.

(Laughter)

**Hon. Speaker:** Mheshimiwa Kingori asante. Mheshimiwa Kituku.

**Hon. Kituku:** Asante Bi. Spika. Ninashukuru Mheshimiwa Eric Musembi, kwa kuleta mswaada ambao ameleta mbele ya hii bunge na niseme ni mswaada mzuri sana ambao ukitekelezwa utakuwa umesaidia watu wa Kalama sana. Bi Spika, hii bunge imepitisha miswada mingi sana na mara mingi waheshimiwa kama si nguvu ya mwili tungekuwa tumeuwawa na *stress* sababu kuna watu ambao wamelala mahali kwa kazi yao. Singependa kusema ni kamati ya *Implementation* ndio haijafanya kazi kwa sababu sisi tukisha pitisha mswaada bunge kupitia *Clerk* wanawasilisha yale maoni waheshimiwa wametoa kwa *Executive* ili waweze kufanya hio kazi.

Lakini hakuna anayeweza kutoa sababu kamili kwanini mambo mengine huwa hayatekelezwi, na ndio kazi yetu kama waheshimiwa tuweze kukodolea wale ambao hawafanyi kazi yao macho kwa vikali sana kwani wananchi wanaumia. Mswaada kama huu ulipitishwa kama mwengine tulijadili hapo mbeleni wa *contracting* wakati wa bunge iliokuwa kwa ward yangu lakini naona kuna kuzembea kidogo.

Hata *machine* za kutoa huo mchanga kwa mabwawa hayo ama kutengeneza mengine mapya, tuko na hizo *machine* lakini hazijaangaliwa vizuri, kwa hivyo naomba waheshimiwa, katika kila kamati mko, tukaweze kuangalia hizi *departments* zote zile ambazo bado hazijaweza kutekeleza mambo ambayo tumeyapitisha ndio wananchi wetu wakaweze kupata maji haswa, kama huu wakati tumebakisha tu kipindi kifupi katika kazi ambayo wananchi wapetupatia.

Kazi ya MCA sanasana ni kazi ngumu kwa maana hana hazina; ni lazima sisi tupitisha mambo halafu sisi tukaweze kuwapatia Governor na mawaziri wake na maChief Officer, wakaweze kufanya kazi. Wakikataa kufanya kazi sisi tunatoa maoni kupitia miswada kama hii, *reports* zingine tunatoa kama zingine tumeweza kutoa siku hii ya leo na halafu tunapatia serikali kufuatilia wale ambao hawajafanya kazi.

Kwa hivyo mheshimiwa MCA huwa ana kibarua kizito sana juu mara nyingi niyeye mnakutana na yeye hapa kwa hapa tu; tutengenezee barabara lakini shida yake, hana hazina yeyote, sio kama wale wengine, lakini sisi tunafanya kazi yetu, ndivyo tunaomba wananchi muendelelee kufuatilia yule ambaye hafanyi kazi yake. Kama ni *executive* lazima mnakutana na wao, kama ni sisi wabunge lazima mnakutana na wao kama siku ya leo, ulizeni kila mmoja kazi yake ili ile haki yako uipate. Asante.

**Hon. Speaker:** Thank you, Hon. Kituku. Hon. Muli.

**Hon. Muli:** Asante Bi. Spika, Waheshimiwa wenzangu ambao wamefika mahali hapa, na wakaaji wa eneo hili kwa kuhudhuria hiki kikao. Langu Bi. Spika ni kusema kwamba ni kweli kwamba mabawa ya sehemu nyingi, sio hapa peke yake yamefurika. Hii ni kwasababu mvua ikinyesha maji inateremka kutoka kule milimani halafu inaingia kule kwa ile mabwawa na baada ya mwaka mmoja mbili unakuta imefurika na imejaa. Serikali yetu ya Machakos ama ya *County Government*, ni kweli kwamba tutaipatia pesa ya kufanya kazi na ukweli usemwe; kuna wale ambao wamelalia kazi yao.

Maanake tunapowapatia pesa ya kufanya kazi unakuta kazi haiendelei, na ndio unaona wakaaji wote wanaanza kulia kwa sababu hawapati faida ya pesa yao. Bi. Spika nasema kama wenzangu kwamba kama ingeliwezekana, huu mswaada ambaye mheshimiwa Eric ameleta, ungekuwa kwa *County* yote ya Machakos.

**Hon. Speaker:** Naelewa kwamba kuna msheshimiwa anataka kuleta msawaada ndio tufanye masahihisho ama *amendment* kwa hii *motion*, kwa hivyo kuna msheshimiwa ako na hilo Jambo? Mheshima Pauline, Mheshimiwa Muli, unaweza kuendelea kuongea baada ya hii *motion* ya ku *amend* maana nimesikia vile inaenda. Kwa sababu inahitajika mabwawa katika kila sehemu ya *County*. Hebu pumzika kidogo tafadhali.

**Hon. Muli:** Thank you, Hon. Speaker.

### AMENDMENTS TO MOTION

**Hon. (Ms.) Mene:** Asante, Bi. Spika.

*I wish to amend the motion by Hon. Musembi as follows:-*

*By adding the words 'all wards in Machakos County' after Kola ward and adding the words 'residents of all wards' after Kola ward.*

*I wish to ask Hon. Museku to second the motion.*

*(Applause)*

**Hon. Museku:** Thank you, Madam Speaker. I do second that motion.

*(Applause)*

**Hon. Speaker:** Shukran Waheshimiwa Pauline and Museku. Nimangalia juu ya *Standing Orders* zetu na nimeona kwa kifungu cha 51 na 52 kinaeleza vile msawaada wa kufanya mabadiliko unafaa kufanywa na kwa vile hakujakuwa wakati wa kutosha ndio tufuatilie huo mpango wa hio sheria, na kwa vile Spika amepewa nguvu ama power, amepewa kibali kukubali usahihisho wa motion chini ya kifungu ya 52(2).

Kwa hivyo ile inaeleza kwamba, *despite paragraph 1*, ile inaeleza kwamba amendment lazime iwe *in writing, the Speaker may in exceptional circumstances allow a member to move an amendment to a motion before the House at any time during consideration of that motion*. Kwa hivyo kupitia kwa hicho kifungu cha *Standing Orders* ya Assembly, nimekubali hao waheshimiwa waweze kufanya amendment kwa sababu ukisikiza vile Waheshimiwa wanaongea ni kwamba hii shida haiko Kola ama Kalama Ward peke yake; iko kwa ward mingi ya county ya Machakos.

Kwa hivyo sasa nitaendelea ndio niweke swala ambalo mtaongea kidogo juu yake kabla ya tupige kura, kama tutabadilisha ama hatutabadilisha.

*(Question, that the words to be added be added, proposed)*

*Hon. Muli was in his feet and he had just come to a stage where he was proposing an ammendment but we needed to do it in a formal manner.* Hon. Muli, unaweza kuendelea. *Remember it is a motion within a motion.* Tutasahihisha ama hatutarekebisha msawaada?

**Hon. Muli:** Asante Bi. Spika. Naunga mkono; kama vile nilikuwa nimesema, kwamba ili kazi ifanyike kwa kaunti yote ya Machakos. Na Bi. Spika nilikuwa nimesema ya kwamba, pesa



huwa tunapeana kama Assembly ya Machakos lakini tukiwapea pesa wale ambao wanatenda kazi---

**Hon. Speaker:** Nauliza Mheshimiwa; turekebishe ama hatutarekebisha.

**Hon. Muli:** Turekebishe.

**Hon. Speaker:** Okay. Tukimaliza juu ya kurekebisha basi utaendelea. Mheshimiwa yule anataka kuongea juu ya kurekebisha? Mheshimiwa Muthoka alafu Mheshimiwa Mueni na hio itakuwa brief kwa sababu hakuna mambo mingi.

**Hon. Muthoka:** Asante Bi. Spika. Naunga mkono turekebishe kwa sababu Madam Speaker, unajua tulipitisha mswaada wa *Climate Change*, na *Climate Change* inahusu Machakos County na kuna pesa mingi sana iko hapo, tumepatiwa na World Bank, sasa tunaomba serikali ya Mutua.

**Hon. Speaker:** Mheshimiwa, serikali si ya Mutua; ni yako pia.

**Hon. Muthoka:** Tunaomba *side* ya *Executive* wafuate sheria kwa sababu tukichukua hii ksh. 1.2 B tumepatiwa na World Bank na tuiweke kwa maji, watu wote wa Machakos watapata maji, hatutaongea kuhusu maji. Kwa hivyo naomba turekebishe kwa sababu tuko na pesa, hakuna kirefu kisicho kuwa na mwisho, sitaki kuongea mambo ya *implementation* sana sababu serikali ishahindwa ku *implement* vitu sana kwa hivyo naomba turekebishe kwa sababu kuna pesa ya County yote. Asante.

**Hon. Speaker:** Mheshimiwa Mueni; kwa kurekebisha mswaada.

**Hon. (Ms.) Mueni:** Asante Madam Speaker. Naomba turekebishe kwa kuweka maji kila mahali ili iwache kuteremka ikienda India Ocean and *as I said another time, I was talking to our Governor starting this Government in 2013 and he told me that I will not see any water going to the Indian Ocean but that is still going on. So you have done very well to say that turekebishe hii kwa sababu kina mama they are the ones who look for water. You will have done well to say that they will not be going to look for water and as Mheshimiwa Alice has said God will pay you for this and if we give you seat for Governor---*

**Hon. Speaker:** Mheshimiwa Mueni you are out of order. Stick to the motion on the Table.

**Hon. (Ms.) Mueni:** People will stop going to fetch water. Thank you, Madam Speaker.

**Hon. Speaker:** Hon. Ndawa, kwa kurekebisha mswaada.

**Hon. Ndawa:** Thank you, Madam Speaker. L looking at the mood of the House, everybody is supporting that we *turekebishe* hio motion. *Kwa hio naomba uweke swali.*

**Hon. Speaker:** *Mheshimiwa* Ndawa be orderly; you do not direct the Chair on what to do. You either support or not.

**Hon. Ndawa:** I am supporting that we ammend the motion. Thank you, Madam Speaker.

**Hon. Speaker:** Hon. Members, I will call upon the mover of the motion to reply.

**Hon. (Ms.) Mene:** Asante Bi. Spika. Waheshimiwa wabunge wamechangia na nithihirisho kamili ya kwamba watu wote wangependa huu mjadala ubadilishwe uwe tunaongea juu ya Machakos *County* yote. Asante Bi. Spika.

**Hon. Speaker:** Asante Bi. Pauline.

*(Question, that the words to be added be added,  
put and agreed to)*

*(Question of the Motion as amended proposed)*

*(Question of the Motion as amended put and agreed to)*

So, Hon. Members, now that you have voted to ammend the motion so that the de-silting and reticulation of water from the existing dams is in all the wards of the County, remember now those who want to contribute to this motion you will be adressing the issue of the works being done in every ward of the County. Any Member who wants to contribute to that? Hon. Musau and then Hon. Kieti.

**Hon. Musau:** Asante Bi. Spika kwa wakati ulio nipa, cha kwanza ni kusema shukurani kwa Mheshimiwa Eric kwa mswaada wa marekebisho. Cha mhimu sana, maji ni uhai, na maji ikiwa uhai, wananchi wa Machakos kwa jumla, wanateseka kukiweko na mabwawa ya kuteseka, mabwawa yaliyotengenezwa na wakoloni, mengine yametengenezwa na County yenyewe, na kama yatakuwa *de-silted Madam Speaker*, tutakuwa na maji ya kutosha. Na hii maji itasaidia wananchi wote, hii maji ikisambazwa tutapunguza ule mwendo wananchi na haswa kina mama wanaenda kutafuta maji.

Cha muhimu ni kuona hata kabla mabwawa mengine hayajatengezwa, kwanza haya yatengezwe, yatolewe mchanga na hii maji isambazwe *such that* ikiwezekana, hakuna mwananchi ataenda kilomita tano kutafuta maji. Kwa hivyo changu ni kuuliza sana our *Executive*, sisi kama wabunge wa Machakos, tumefanya kazi yetu, sasa jukumu ya kutekeleza iko upande wa *Executive*. Serikali iko na vitengo mbili; kitengo cha *County Assembly* ambacho ni sisi kazi yetu ni kupitisha, upande wa utekelezaji ni *Executive*, sisi tumefanya kazi yetu. Sasa ni wakati wa *Executive* na wao, tumewapatia, tumepitisha, tumewapatia *budget* nao watekeleze ndio wananchi waweze pata maji. Asante sana, *Madam Speaker*.

**Hon. Speaker:** Shukurani Mheshiwa Musau. Mheshimiwa Kieti.

**Hon. Kieti:** Asante sana Bi. Spika kwa kunipa hii nafasi. Nataka kuanza kwa kushukuru Mheshimiwa Musembi na Mheshimiwa Pauline ambao ndio wametupatia huu mjadala ambao tunajadiliana. Nataka kusema 2018 nilileta hoja kama hii katika bunge, nilileta motion ya *de-silting* ya *dams* zetu na *reticulation* ama kusambaza maji katika *our households* na hio hoja ilipita katika bunge na mpaka sasa hatujaona kazi ikitekelezwa kama vile wabunge walipitisha.

Kwahivyo yangu ilikuwa niseme ya kwamba hoja kama hii ilikuja kwa bunge na tukapitisha na ni ombi yangu, kwa maana yale maombi yangu ambayo nilikuwa nimeweka katika hiyo *motion*, ni kama yale ambayo tuko nayo siku ya leo. Madam Speaker, ningeomba, *Executive* waweze kusukumwa wafanye kazi yao kwa vile pesa tumewapatia katika *budget* mbalimbali, zile *budget* zimekuja hakuna ile *budget* ambayo hatujawahi tenga pesa ya maji na ukitembea katika Kaunti yetu utapata sehemu nyingi ziko na shida ya maji.

Sehemu kama hii ya Kola ni sehemu Bi. Spika nilitembea nikiomba kiti ya KNUT, nilikuwa nimesimamia mashule pande hii kutoka hapa mpaka Athi River na Kathiani na ni sehemu iko na shida mingi ya maji na vile vile sehemu ya Athi River ni sehemu nimetembea sana. Kwa hivyo naombo kwamba *wards* zote kwa vile ziko na shida sawa ya upunguvu wa maji, *Executive* waweze kuangalia ile pesa ambayo tumewapatia na sana sana ile pesa ya *Climate change* Mheshimiwa Kingori ameongelea ambayo tumepatiwa kama msaada.

Ni pesa ambayo ingesuluhisha hii shida ambayo tunaongelelea siku ya leo. Kwa hivyo ni ombi langu vile *budget* itapitishwa ya maji iweze kutekelezwa ndio iweze kusaidia watu wetu katika maeneo yale wanaishi. Asante sana, Bi. Spika.

**Hon. Speaker:** Asante sana Mheshimiwa Kieti, Mheshimiwa Kasyoki, na tukiwa hapo mheshimiwa Musembi ujitayarisha kujibu.

**Hon. Kasyoki:** Asante sana Bi. Spika. Nimesimama kuunga mkono huu mswaada umeletwa na Mheshimiwa Eric. Yangu ni kusema zile *dams* ziko kwa *wards*, kama *our County Government* ingechukua zile pesa tumewapatia wangeweza kutengeneza hio maji iende kila mahali kwa ajili sehemu ya Ukambani maji iko shida sana, na mvua ikinyesha, mnapata maji nyingi badala ya kutusaidia inaenda Indian Ocean.

Kwa hivyo ningeomba tu *our Executive* iweke hii kitu maanani ihakikishe imefanya hata kama sio nyingi kwa ajili kila ward inajua zile sehemu zake ziko na shida ya maji. *At least* wawe wakitufanyia hata kama ni *dam* moja kwa kila *ward*; ward zote arobaini itakuwa kitu ya maana sana na wananchi watahukuru. Ni hayo Bi. Spika. Asante.

**Hon. Speaker:** Asante Mheshimiwa Kasyoki. Mheshimiwa Musembi, *you reply as the mover of the motion.*

**Hon. Musembi:** Asante sana, *Madam Speaker*, na kwa waheshimiwa wabunge, kwa kuunga mkono mjadala wangu na Mheshimiwa Mene, kwa kuleta hio *amendment*. Nimefurahia sana kwa kunishika mkono. Ile kitu naweza sema kwa kusema ukweli mkisikia nimeleta huu mjadala, sisi kama wakaazi wa Kola wameteseka sana. Tumejaribu kuchima *boreholes* tukisaidiana na idara ya maji ya *County* lakini kila tunapochimba *borehole* maji haipatikani. Pale mahali kidogo tunapata *borehole* unapata huwezi pata lita elfu kumi mfululizo; inakauka.

Sasa hata ukienda kwa *boreholes* zenye ziko kwa ward ya Kola unapata watu wamefunga laini sasa unashindwa hii ni kazi gani. Mtu anakaa pale kutoka asubuhi mpaka saa nne, huyo ni

mama ako na mtoto, baba ameacha kazi zake, watu hawafanyi kazi ila ni maji tu. *So Madam Speaker*, sisi kama bunge tutaendelea kuangalia hio maneno yote imepitishwa ndio wakaazi wetu waweze kupata maji na sababu maji ni uhai, tukipata maji tutafanya ukulima pia tupate chakula na tuwache kuombaomba *donors* na vitu kama hizo. *So* nashukuru sana na Mungu awabariki. Asanteni.

*(Applause)*

**Hon. Speaker:** Thank you, Hon. Musembi.

*(Question put and agreed)*

REPORT ON DEPARTMENTAL REPORT FROM THE DEPARTMENT  
OF TRANSPORT, ROADS AND PUBLIC WORKS FOR 2019/20

**Hon. Speaker:** Hon. Members, before we proceed to this Order, I want to go back to Order No. 8 and direct that the resolution you have just passed is committed to the Environment, Lands, Energy and Natural Resources Committee for processing and reporting to this House on or before the 25th of August, 2021.

Hon. Mbevi, or any member who is standing in for Hon. Mbevi. I can see Hon. Irene Mbivya.

**Hon. (Ms.) Mwendu:** Asante, Bi. Spika.

Hon. Speaker, that aware that the County Assembly's oversight function is one of the cornerstones of democracy;

Aware that oversight is a means for holding the County executive accountable for its actions and for ensuring that it implements policies in accordance with the laws and budget passed by the County Assembly;

Hon. Speaker, acknowledging that Article 183(3) of the Constitution of Kenya, 2010 provides that the County Executive Committee shall provide the County Assembly with full and regular reports on matters relating to the County;

Further aware that Article 185(3) states that the County Assembly while respecting the principle of separation of powers, may exercise oversight over the County Executive Committee and any other County Executive organs;

Hon. Speaker, cognizant of the fact that Standing Order 190(5)(b) mandates sectoral Committees to study the programme and policy objectives of the departments and the effectiveness of the implementation;

Aware that the Committee on Transport, Roads, Housing and Public Works received the Departmental Report for the FY 2019/20 from the Department of Transport, Roads and Public Works;

Further aware that the Committee conducted site visits to ascertain the status of the projects indicated in the report, held meetings with the Chief Officer and compiled a report;

Hon. Speaker, I wish to move the motion that this Hon. House discusses and approves the Transport, Roads and Public Works Departmental Report for the FY 2019/2020.

I wish to call upon Hon. Musyimi to second my motion.

**Hon. Speaker:** Thank you, Hon. Irene. Hon. Musyimi.

**Hon. Musyimi:** Thank you, Hon. Speaker. I do second.

**Hon. Speaker:** Hon. Members, you remember how to second when you wish to comment; you remember? Hon. Members, so let us continue Hon. Irene.

**Hon. (Ms.) Mwende:** Thank you once again. *Nitasoma hii ripoti japo ni refu kidodo mtanivumilia.*

**Hon. Speaker:** *Utatafuta jinsi ya kufupisha bora upate kutuelezea yale ya maana. Yale mengine waheshimiwa wanaweza kusoma baadaye. Na ukumbuke waheshimiwa wako na hii ripoti tayari.*

**Hon. (Ms.) Mwende:** Thank you. So you have the report with you, I will go straight away to the matter under consideration today.

### 3.1 OVERALL BUDGET FOR THE FY 2019/20

Hon. Speaker, in the financial year 2019/20 the County Assembly approved the Department's total budget of Ksh. 1,520,088,660 comprising of Ksh. 159,286,031 as the recurrent budget and Ksh. 1,360,802,629 as the Development budget. These amounts are based on the revision of the budget through the two Supplementary Budget Appropriation Bills with the latest being done on 22<sup>nd</sup> June, 2020.

The Development budget allocation is inclusive of a conditional grant from the National government revenue (Road Maintenance Fuel Levy Fund) of Ksh. 363, 636,021. The breakdown per program is as follows;

#### Recurrent Budget

S/NO	PROGRAMME	AMOUNT ALLOCATED FOR THE FY 2019/2020
P01	Headquarters Administrative Services	113,734,699
P02	Road Development and Management	1,000,000
P03	County Government Buildings	2,254,370
P04	County Fleet Management	42, 296,662
	<b>TOTALS</b>	<b>159,286,031</b>

#### Development Budget

S/NO	PROGRAMME	AMOUNT ALLOCATED FOR THE FY 2019/2020
P01	General administration and support services	52,000,000
P02	Road Development and Management	924,219,241
P03	County Government Buildings	304,583,388
P04	County Fleet Management	80,000,000

<b>TOTALS</b>	<b>1,360,802,629</b>
---------------	----------------------

#### 4.0 COMMITTEE FINDINGS

Hon. Speaker, the Committee interrogated the above reports and found out the following;

1. The report from the Department indicated that Ksh. 260M was received from Road Maintenance Fuel Levy Fund and fully spent. The report from the Controller of Budgets indicated that Ksh. 220M was the actual receipts for the said Programme.
2. Ward Emergency Projects were initiated in the FY 2018/2019 and appeared in the Departmental Report for FY 2019/2020.
3. The grading Programme was not quantified on the actual expenditure but on the Kilometers covered.
4. Works for a number of County Government Buildings have stalled and others had low absorption rate despite having a budget allocation.
5. The amount spent on motor vehicle insurance exceeded the approved budget on the same vote for the FY 2019/2020.
6. The amount spent on maintenance of equipment and plant exceeded the approved budget on the same vote for the FY 2019/2020.
7. The actual expenditure on fuels, lubricants and oils was Ksh.24M against a budget allocation of Ksh. 80M
8. That the Department of Roads, Transport and Public Works was among the Departments with the highest Development expenditure in the County with the major projects being Construction of County Government Buildings and Maintenance of Mitaboni-Ndulu-Lia Road at costs of Ksh. 218,276,065 and Ksh. 135,563,057 respectively. This is according to the report from the Office of the Controller of Budget.
9. The Expenditure to Exchequer Issues for the Department was Ksh. 782,680,000 against Actual Exchequer issues of Ksh. 1,087,210 hence an absorption rate of 57.5 per cent.
10. The Controller of Budget report indicates an expenditure of Ksh. 135,563,057 against an allocation of Ksh. 193, 673,220 for maintenance of Mitaboni- Ndulu- Lia Road. The report from the Department of Transport, Roads and Public works does not have such a project with such an allocation and expenditure.

#### 4.1 SITE VISITS

Hon. Speaker, further the Committee conducted site visits to selected roads projects, ongoing public works projects and the County Garage.

The following were the findings of the site visits:

1. That as at the date of the site visit on 26<sup>th</sup> October, 2020, the culverts on Syokimau roads had not been installed. This contradicted the report from the Department on the status of KRB projects as at 12<sup>th</sup> August, 2020.
2. The status of Tumba-Kwa Moni Road in Mumbuni North Ward indicated that the works were completed. During the site visit the Committee noted that the protection works and rock fill were not well done and the estimated status at 50

- per cent was wrongly reported. This again contradicts the report from the Department.
3. Nothing had been done on Kamweani Road in Kithimani Ward. The report from the Department indicated that installation of Culverts and protection works had been done to satisfaction.
  4. The Committee also noted that only one culvert had been fixed on Kithito-Makweti- Kinyatta Road in Ikombe Ward. The report from the Department indicated that installation of culverts and protection works had been done to satisfaction.
  5. The Committee also noted that the following buildings had stalled;
    - a. Commercial Development (Mixed use) stalled at 10 per cent.
    - b. Community Recreation Centers stalled at 6.5 per cent.
    - c. Office Block 12 storey stalled at 6.5 per cent.

#### 4.2 DISCUSSION WITH THE CHIEF OFFICER

Hon. Speaker, Article 195(1) of the Constitution of Kenya, 2010 stipulates that “a County Assembly or any of its committees has power to summon any person to appear before it for the purpose of giving evidence or providing information. Section 39(2) of the County Governments Act, 2012 states that “a committee of the County Assembly may require a member of the executive committee to—

- (a) Attend or appear before the committee; and
- (b) Answer any question relating to the member’s responsibilities.

Further Section 18(1) of the County Assemblies Powers and Privileges Act, 2017 states that “a County Assembly or its committees may invite or summon any person to appear before it for the purpose of giving evidence or providing any information, paper, book, record or document in the possession or under the control of that person and, in this respect, a County Assembly and its committees shall have the same powers as the High Court as specified under Article 195 of the Constitution.

This Committee invited the Chief Officer, Department of Transport, Roads and Public Works for a meeting on 26<sup>th</sup> October, 2020. The invitation was through a letter Reference No. (MKSCA/ PCS/CMM/TRP/VOL.3/61) dated 19<sup>th</sup> October, 2020.

From the discussion with the Chief Officer, the Committee found out the following:

1. That the difference of Ksh. 40M noted by the Committee in the Exchequer issues of Ksh. 220M against actual Expenditure of Ksh. 260M was amongst funds brought forward from the FY 2018/2019.
2. That the reason why Ward Emergency Projects meant for the FY 2018/2019 appeared in the Departmental Report for the FY 2019/2020 was because the projects were initiated towards the end of the FY 2018/2019 and completed in the FY 2019/2020.
3. The project indicated in the report of the Controller of Budget as Maintenance of Mitaboni-Ndulu-Lia Road as done at a cost of Ksh. 135,563,057 was wrongly reported but instead that amount was utilized under road maintenance under Kenya Roads Board Conditional grant.
4. That the Department was in the process of terminating contracts for all the stalled County Government buildings.

### 5.0 COMMITTEE OBSERVATIONS

Hon. Speaker, based on the reports, site visits and discussion with the Chief Officer, the Committee observed the following:

1. That distribution of KRB projects across the wards since FY 2017/2018 has never been fairly done. This has seen some wards getting an annual allocation of Ksh. 15M while others gets as low as an annual allocation of Ksh. 1M
2. That generally the grading roads program is poorly coordinated because fueling of graders is not consistent and maintenance of the roads' project equipment takes a long time hence inconveniencing the whole program.
3. That the Department of Transport, Roads and Public Works had an absorption rate of 57.5 per cent on development budget for the Financial Year under consideration. This is quite low compared to the expected output in terms of grading, installation of culverts, murraming, maintenance of graders and all other related road works. The Department of Transport, Roads, Public Works stated that the payment processes for certificates raised is done by the Department but the final payment is done by the County treasury and no report is generated back until the financial year lapses.
4. That there are variances between the status of roads as indicated on the Departmental report for the FY 2019/2020 and the real status of the projects at ward level. This is justified by the site visit reports by the Assembly Committee on Transport, Roads, Housing and Public Works. This is a clear indication that the Area MCA is not involved in the road works done by the Department hence high chances of paying for substandard works.
5. That the project in the report of the Controller of Budget indicated as maintenance of Mitaboni-Ndulu-Ini Road is a collection of projects done by the Kenya Roads Board conditional grant in various locations in the County. The Committee observed that the report of the Controller of Budget clustered all the roads under this project. This is misreporting because there was no such a project done by the Department with such actual expenditure.

### 6.0 COMMITTEE RECOMMENDATIONS

Hon. Speaker, this Committee hereby makes the following recommendations:

1. Article 10(2)(b) of the Constitution of Kenya, 2010 provides for the National values and principles of governance amongst them being human dignity, equity, social justice, inclusiveness, equality, human rights, non-discrimination and protection of the marginalized. Distribution of KRB roads projects should be done equitably. The Committee recommends that in the FY 2021/2022 priority should be given to wards that have not benefitted much from the allocation.
1. The Department of Transport, Roads and Public Works should capitalize on result-oriented programs rather than process-oriented programs. For instance, in the road-grading program, distance graded should be used as an indicator and not the fuel consumed. This is because the Committee noted that there is no integrity on the usage of the fuel cards.
2. Departments should have an end-to-end use on the payment processes of services rendered and goods delivered. This way a department will be able to assess its performance quarterly and work towards a better absorption rate.



3. The variance between the real status of road works done and reported status is a clear indication that the Area Member of County Assembly is not consulted during planning and execution of the projects. The Committee recommends that Members of the County Assembly should be involved while identifying the projects since they represent the electorates pursuant to the provisions of Article 1(3) of the Constitution of Kenya, 2010.

#### 7.0 CONCLUSION AND ACKNOWLEDGEMENT

Hon. Speaker, allow me to thank the Department of Transport, Roads and Public Works for submitting the Departmental performance report for the FY 2019/20 according to Article 183(3) of the Constitution of Kenya, 2010. I wish to appreciate the Committee Members for their dedication during site visits, committee sittings and compiling of this report.

Hon. Speaker, the Committee is also grateful to the Office of the Speaker and that of the Clerk to the County Assembly for the continuous and relentless support received as it discharged its oversight mandate.

It is therefore my duty, on behalf of the Transport, Roads, Housing and Public Works Committee to table this report and recommend it to this honorable house for consideration and adoption. Thank you, Hon. Speaker.

**Hon. Speaker:** Thank you very much, Hon. Irene.

*(Question proposed)*

Hon. Members, I invite you to debate the motion. Hon. Mitaa.

**Hon. Mitaa:** Asante Bi. Spika, kwa nafasi ambayo umenipatia kuchangia hii ripoti ya kamati ya idara ya mabarabara. Naomba nishukuru hio kamati kwa kazi ile wamefanya na pia nishukuru maanake ripoti yenyewe imekuja wakati ule tunafanya kikao na wananchi.

Bi. Spika, ni vizuri mwananchi mwenye kulipa kodi apate nafasi ya hizi ripoti kwa maana zinaonyesha vile serikali ya ugatuzi inafanya kazi. Kama ilivyotangazwa awali, kazi ya MCA ni tatu na hii ripoti imeelezea mahali MCA anatakikana ashikilie katika uongozi wa serikali za ugatuzi.

Bi. Spika, ripoti imeonyesha wazi kwamba waliopewa nafasi katika idara ya mabarabara, kazi wanaofanya haifikii kiwango inayotakikana kwa mwananchi wa Kaunti ya Machakos. Ukisikiza ripoti kama wodi ya Ikombe umesikia waskisema *culvert* ni moja na barabara ya Mitaboni ambayo mwakilishi wa hio wodi amekua akiulizia mahali imefikishwa kwa sababu ukiangalia kwa ripoti barabara iko lakini ukienda mahali hio barabara inatakikana kuwa hauipati.

Langu ni kusema tutatilia mkazo tuhakikishe zile fedha zimetengwa kutengeneza barabara na si hizo peke yake, idara zote katika serikali ya Machakos, tutatilia mkazo tuone hizo pesa zimetumika katika njia itaweza kufikia mwananchi ndio naye apate kufurahia matunda ya serikali za ugatuzi.

Bi. Spika, katika hii ripoti tumeona fedha pia ni kama zimetumika vibaya, tutafuatilia pia tuhakikishe wale wanaweza kuwa badala ya kufanya kazi wameweka pesa kwa mfuko, zile idara za uchunguzi zitafanya kazi na hatimaye mwananchi wa Machakos afikie kupata matunda ya kulipa kodi. Bi. Spika, kila wadi tuko na hizi shida.

Imesema pia tuko na hio *programme* ya kukata mabarabara; kila mwaka tunaweka kwa bajeti fedha mingi sana lakini ukiangalia vile zile pesa zinavyotumika, saa zingine hatupati majibu. Kwa hivyo tutatilia mkazo tuone zile pesa zote zinapatiwa hizi idara, zimefikia kufanya kazi na kwa kile kiwango kinatakikana.

Kwa hivyo naomba nitilie mkazo hio ripoti na nishukuru waheshimiwa na naomba wananchi wajue kwamba tunajaribu kukaza ndio serikali ya Kaunti ifikie kuhudumia mwananchi kwa ile njia inatakikana. Asante, Bi. Spika.

**Hon. Speaker:** Asante Mheshimiwa Mitaa. Mheshimiwa Museku.

**Hon. Museku:** Asante Bi. Spika kwa hii nafasi. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Irene Mbivya na kamati ya *transport* kwa kulete hii ripoti bungeni. Ie ningetaka kuisitiza ni kwamba hii ripoti imeleta mambo ya muhimu; kuna barabara moja kwenye eneo langu inaitwa Tumba-Kwa Moni road na ukiangalia kwa ripoti yao inaonyesha iko 100 per cent *complete* lakini walipoenda wenyewe waliona imefanywa 50 per cent. Hio barabara iliwekwa *hardcore* na *contractor* akafanya *compacting* na akaenda. Hakuna *side protection works* zilifanywa, hakuna *drainage works* ilifanywa, lakini ukiangalia kwa BQ ambayo lipatiana kwa hii kazi ambayo ilipatiana kwa hii kazi, hizo kazi zote zilikuwa zifanyike.

Hii ni kumaanisha ya kwamba wenye wanaenda kufanya *approval* ya hizi vitu, kama hawahusishi waheshimiwa na *Project Management Committe (PMC)*, lazima kuwe na *development committee* katika wodi na watu wanaofaa kuwa wakiangalia miradi ambayo inafanywa na serikali na kusign off maradi ukiisha. Kamati ambayo imechaguliwa ya kuangalia kwamba hio *project* imefanyika kulingana na vile inapaswa kufanyika.

Katika serikali yetu ya Machakos, hii PMC nimeona haijafanya kazi kabisa katika hii miaka yote tumekaa hapa. Ukienda eneo la Makueni utapata inafanya kazi sana hakuna *contractor* anaweza lipwa kabla ya PMC kuhakikisha wameweka sahihi na kusema kwamba hio kazi imefanyika.

*Madam Speaker*, jambo ingine ningependa kuongea juu yake ni kwamba tumeona kuna mwelekeo wa serikali kuweka pesa nyingi kwa barabara fulani ambayo inapitia wodi fulani halafu zile wadi zingine hazipati kitu. Kwa hii bajeti inakuja kama *member wa budget committee* tumekuwa tukijadiliana kwamba kuna *proposal* ambayo imekuja ya kutengeneza *dual carriage way* kutoka Kyumbi hadi Machakos town. Iwekwe lami 16 kilometers, *airstrip* itenengenezwe Peoples Park uko mbele na tunajiuliza, kama huku mashinani watu mabarabara zao hazipitiki na tuende tuwaambie tunaweka 800 milioni kuweka *dual carriage*, kazi ambayo inafaa kufanywa na Kenya National Highways Authority (KeNHA) hio itakuwa ni haki kweli?

Hizo hela zinafaa kutolewa uko zikuje tuweke *murrum* zile barabara wananchi wetu wanapitia; tuweke pia *bridges*, na sio kutumia pesa yote kuweka mahali fulani maanake huwa zinawekwa huko ndio zionekane vyenye zitolewa huko. Zikitandazwa kila mahali kila mwananchi apate itakuwa ni ngumu kutoa Bi. Spika. Kwa hivyo sisi kama Kamati tumesema kwamba hatutaruhusu pesa iwekwe katika barabara moja pesa nyingi badala ya kupelekwa katika wadi zote wananchi wote waweze kufaidika.

Hii report imenote hizo vitu; ukiangalia vile wameweka orodha ya mabarabara unaona Muthini-Vota road 105 million; hio 105 million ungepatia wadi zote kila wadi ingepata million tatu. Na milioni tatu, kila wadi ingekata barabara moja na iweke *murrum* lakini inapeleka ward moja na unaweka 105 million. Kwa hivyo kama Bunge, tuhakikishe ya kwamba,

pesa ambazo zimepeanwa kwa mabarabara zigawanywe usawa wodi zote ndio watu wetu waweze kunufaika.

Pia, hii makosa ambapo *a project is indicated in the controller of budget as maintenance of Mitaboni-Ndulu-Lia road done at a cost Ksh. 135 million was wrongly reported but instead the amount was utilized under roads maintenance under Kenya Roads Board conditional grant.* Ukisema kwamba the *Controller of Budget* ame *mis-report* na yeye ndiye ako na *requisitions*, hii lazima iangaliwe Bi Spika. Tukisema kwamba hio pesa haikuwekwa kwa barabara n iliwekwa pahali ingine, CoB huwa anatangeneza hizi vitu akiangalia *requisitions* ambazo zimetengenezwa.

Kwa hivyo ni lazima tuangalie hii *requisitions* ilifanywa ya Ksh. 135 million labda ilifanywa kwa barabara ya kwako na haikufanya kazi kwa hiyo barabara. Kwa hivyo ningepomba Kamati tuchunguze hio tuone *was it KRB* ama ni pesa ilimea miguu na ikaenda. Asante Bi Spika.

**Hon. Speaker:** Shukrani Mheshimiwa Museku. Hon. Eric.

**Hon. Musembi:** Asante sana Bi Spika. Hii *Committee* imefanya kazi nzuri inayoongozwa na Hon. Irene. Hii ripoti kama kamati mnapaswa kuiangalia sana; kwa mfano, mafuta ikiwekwa kwa tingatinga inafaa ipime zile kilomita zimekatwa si tingatinga imewekwa mafuta kiasi gani. Kama barabara inakatwa ni mahali tambarare, huwezi linganisha na barabara ikitengenezwa kwa milima. Tumeona pia kwa ripoti imesemekana *most of the machinery* kazi ni kuharibika. Hata ukikula *chips* na uangushe *toothpick*, utadungwa. Sasa hio ni kazi gani na pesa imetolewa?

Kwa hivyo nawaomba kama Kamati muangalie hio maneno ndio tupate barabara zetu ziko sawa na watu wetu watembee vizuri. Hasa hasa huku Kola ni milima na hii maneno ya barabara kupeanwa *contract* na ripoti inasema imetengenezwa lakini ukienda kwa ground unapata vitu ni tofauti.

Kwa mfano kuna barabara inaitwa Kamuuani-Kya Munyuu; niliangalia kwa ripoti inasema iko *100 per cent complete* ilhali mimi kuenda pale napata *culvert* iliwekwa nusu na ingine ilibebwa na mvua na nikashikana na mwananchi tukaweka *materials* na kwa ripoti inasema *100 per cent complete*. Kusema ukweli watu wangu, *tukeea mwene nthi ata indi* (what shall we tell the taxpayers). Kwa *committee*, kazi kwenu lakini mnaifanya kazi nzuri. Asanteni.

(Applause)

**Hon. Speaker:** Thank you, Hon. Eric. Mheshimiwa Muthoka.

**Hon. Muthoka:** Asante Bi Spika kwa kunipa fursa tena tujadili huu mswaada wenye uzito wa barabara. Watu wetu wameumia sana na unaona kabisa kuna pesa nyingi sana hii bunge inapatia serikali ya county ya Machakos. Sisi tukiwapatia pesa, wao ndio wanaenda *kuimplement*. Tulipeana *one point something billion* pia kuna pesa ya KRB *three hundred million and something* na unajiuliza kama *Chief Officer* wa roads anaweza fanya mistake ya Ksh. 135 million na hii ni pesa mingi sana.

Na hiyo mahali wanasema Mitaboni-Ndulu-Lia road ni kilomita moja inatoka Mitaboni inafika kwa mtu anaitwa Joshua Kiilu hata Spika anamjua na hio ni *1.2 kilometers*. Na si yeye aliona hii makosa ni CoB ameona. Kwa hivyo hii 135 milioni inapaswa kuangaliwa sana ilienda wapi? Tufuatilie tujue. Kwa hivyo Mheshimiwa Ndawa nataka kukutuma---

**Hon. Speaker:** Mheshimiwa Muthoka, *you are out of order.* Unatuma Mheshimiwa Ndawa akafanye nini na kwa sababu ako na cheo gani?

**Hon. Muthoka:** Kwa sababu yeye ndiye---

**Hon. Speaker:** Hapana usijibu. *You are out of order.*

**Hon. Muthoka:** I withdraw.

**Hon. Speaker:** That is good.

*(Laughter)*

**Hon. Muthoka:** Nasema hii ni maneno tunafaa kuangalia na tuogope Mungu si binadamu. Tukipeana hii pesa tunaomba serikali itumie kwa njia inayofaa. Unaona kuna ward inapatiwa 15 million za barabara na ingine one million. Imetumia criteria gani ya kupeana Mua ward 15 million na Kalama inapatiwa one million. Tunaomba serikali yetu ifuate haki na kama Mua inapatiwa 15 million Kalama pia ipatiwe 15 million ndio tuwe na usawa. Kwa sababu ukisema unafinya Mheshimiwa, haufinyi mheshimiwa unafinya watu wa mungu.

Kwa hivyo tunaomba serikali yetu iwe *serious* hio mwaka moja imebaki lakini hakuna shida, kutoka 2022 tutaonesha vile kazi inafanyangwa. Asante Bi. Spika.

**Hon. Speaker:** Mheshimiwa Nyanzi; asante Mheshimiwa Muthoka.

**Hon. Nyanzi:** Asante Spika kwa kunipatia hii nafasi. Mimi ni mzaliwa wa hapa na nimekuwa *councillor* miaka mingi na najua kila kitu lakini kitu moja nimesikia kwa hii bunge tunayo ni ya maana sana kwa wananchi wa Kalama. Ile kitu itaokoa watu wa *county* ya Machakos ni kujua kwamba, Spika ametembea Yatta na kila pahali akisikiza kila kitu iko kwa *ground*. Come 2022 ndio itaokoa nyinyi kuchagua huyu awe Gavana wa Machakos.

**Hon. Speaker:** Mheshimiwa Nyanzi, *I am going to name you.* Mheshimiwa Nyanzi---

**Hon. Nyanzi:** Nimesikia.

*(Loud consultations)*

**Hon. Speaker:** Order *Mheshimiwa Nyanzi.* Hon. Members, Order! Let us stick to the motion on the Table; let us not go out of order.

**Hon. Nyanzi:** Sorry, Speaker. *Nilikuwa nataka kusema ya kwamba hapa Kalama, haujasikia ikisomwa; Kyangala na Kalama, tuko na shida moja kubwa sana. Headquarters yetu iko Kyangala, na tuko na barabara moja ambayo inapita kutoka hapa mpaka Kyangala na Makaveti na hio barabara haipitiki. Hio barabara ikitengenezwa na sana iwekwe lami watu watakuwa na urahisi kupita. Wafanyikazi wa serikali wote wanakaa Muumandu ndio iko lami na*

*ofisi za DC ziko uko. Kwa hivyo nimesimama kuuliza kama hio inaweza kuwekwa ili barabara hii ya Kalama na Kyangala iingie.*

*Ile ingine niliinua mkono niongee ni juu ya projekts za Kyangala na nitapatia Clerk at the Table kwa sababu hatuna masaa ya kusoma hio hili wasome za Kalama zile zinafaa kufanyiwa kazi. Asante sana.*

**Hon. Speaker:** Asante Mheshimiwa Nyanzi. Mheshimiwa Mwikali.

**Hon. (Ms.) Mwikali:** Asante, Bi Spika. Madam Spika, ile kitu inaudhi sana kwa kuwa mimi ni *Member* wa hio Kamati ambayo imelete hii ripoti; inaudhi sana kwa kuwa sisi tunahudumia wananchi ambao wametuleta kwa hiki kikao cha bunge. Ukiona waheshimiwa wanakasirika mpaka mtu anasema tutafute serikali ingine mwaka ujao ni hii ripoti imekasirisha wananchi.

Kuna kitu moja imetusumbua sana. Madam Spika nilikuwa nimeketi kando ya mheshimiwa wa Mitaboni na ripoti imesema ya kwamba hio barabara moja ambayo *it is less than one kilometer I am witness because I come around that area*. Hio barabara imepewa pesa nyingi na Mheshimiwa ambaye wamemchagua hapo hajajua na hajaona ikifanyiwa na pesa imetumika Bi. Spika.

Hio inaudhi na kuna watu sijui wanaogopa nani; lakini kwanini unaweka pesa nyingi kiasi hicho badala ya kusaidia wananchi na barabara zimeharibika wewe hata hauogopi Mungu. Mtu ni kama shetani huyo, *Madam Speaker, and we are here to condemn such an act because it is very unfair for county government and I condemn the words that where condemning the roads committee here.*

*Madam Speaker that report comes from the roads committee which was just condemned by another Member in this Chamber. The road committee checks on our peoples expenditures and then we are shocked to see kuna wards ambazo they are so special ore than zingine. Hawa wananchi wote wamechagua hio serikali ya county government na wako na haki ya kufanyiwa biashara zao, barabara zao, wanawake wajawazito wapate barabara nzuri za kupelekwa mahospitali, na hospitali pia zitengenezwe vizuri na hio county government. Yule ako Kalama, yule ako Mananja yule ako Yatta, wote wanahitaji services.*

*Madam Speaker we condemn that act in the strongest terms possible and ask, because this County Assembly is like a High Court, such acts cannot be forgiven; they should be taken to the highest seat where Madam Speaker you sit and then we judge and those who have done that should be taken to court to be jailed miaka yote ndio wananchi wajue hii bunge inafanya kazi. Thank you, Madam Speaker.*

**Hon. Speaker:** Thank you, Hon. Margaret. Let me finish on this side, Hon. Helen then Hon. Kisini.

**Hon. (Ms) Ndeti:** Thank you, Madam Speaker. *Nataka kucongratulate committee ya transport wamejaribu kuandika hio ripoti kwa sababu hawajaficha chochote wametuambia vile mambo iko kwa ground. Nataka kusema kwa ufupi, hio department ya transport in Machakos County is always given the highest allocation lakini ukifuata ile absorption rate ama vile hizo pesa zinatumiwa hawatumi; hakuna kazii imefanywa pesa tumewapatia lakini hakuna kazi wamefanya na projects zile wanasema wamefanya, hata hazijaisha.*

*Kwa hivyo naomba serikali ya Machakos, hii ndio mwaka ya mwisho na tumekuwa hapa miaka nne mwaka wa mwisho projects zote walikuwa wameanzisha pesa zile tunawapatia na hii bajeti ya hii mwaka waangalie zimalizike. Asanteni.*

**Hon. Speaker:** Thank you, Mheshimiwa Helen. Mheshimiwa Kisini.

**Hon. Kisini:** Asante sana Bi Spika kwa kunipatia nafasi mara ya pili. Nataka kupongeza *committee* ya *roads* ambayo imeongozwa na *Vice-Chair* Mwende.

**Hon. Speaker:** Who is Mwende; just Mwende?

**Hon. Kisini:** Hon. Irene Mbivya na nafikiri ako na hio jina pia. *Madam Speaker* ni asante sana. Leo nafikiri hio kamati naipongeza kwa sababu imetupanulia wazi vile pesa ya hio miaka imetumika. Wananchi wale wako hapa na wabunge wenzangu tumesikia ya kwamba imepata *over Ksh. 1.2 Billion allocation* ya kutengeneza barabara zote za kaunti ya Machakos. Leo asubuhi kupitia kwa Mheshimiwa wenu Hon. Winzi, ilisemekana ya kwamba---

**Hon. Speaker:** The name we have is Hon. Eric.

**Hon. Kisini:** Hon. Eric Musembi. *Sorry* kwa kuzoea majina yasiyo *official* lakini Hon. Eric Musembi; alileta mswaada asubuhi akiomba barabara za huku Kola *ward* yatengenezwe na sasa hivi tunawasomea hii ripoti hasa wananchi wa hapa Kola *ward* msikie vile pesa zimetumika. Mmesikia pesa ya magari, tingatinga, mambo ya *motor vehicles* ambayo inatumika kwa hiyo *department* na zile *lubricants* zinatumiwa zinaexceed zile pesa ambazo tumepeana kwa bajeti. Na mkisikia pesa zimetumika zaidi, mbunge wenyu na sisi pia tunacomplain kwamba hakuna kitu tunaona. *So* ni makosa sana kusikia pesa imetumika na hatuoni kazi ile imefanywa.

*Committee* imetuonyesha wazi ya kwamba ile pesa imepeanwa kwa kufanya mambo ya barabara na ikaquote Syokimau, Ikombe, Mitaboni na inasemekana *inaexceed* ama *inacontradict* na hio inatokana na CoB ama yule anaangalia mahesabu. Mmesikia *complaint* ya kwamba sisi MCAs hatuhusishwi kwa kuangalia hio kazi ikifanyika.

Sijui kama hatuhusishwi ndio tufichwe pesa iende ama namna gani; na ndio tunaomba kupitia kwako Bi Spika hio makosa ambayo imeonekana mingi katika hio ripoti na ni *millions of shillings* imetumika iangaliwe wazi kinagaubaga kama kwangu vile tu mmesikia mkienda wa *ward* yangu mabarabara ndio mbaya zaidi na kwangu ni ile mchanga mbaya *clay soil*. Huku kwenu ni afadhali kidogo kwa sababu kukata ni nywee; tinga uko kwetu zimesimama na hazipatikani. Ndio tujue kama pesa imetumika hivyo na vile watu wanateseka ni kwa nini.

Nataka kusema ya kwamba tumesikia *view* ya KRB ambayo saa zingine inatengeneza na *inaqualify* na hio pesa ya KRB inakuja kusemekana kama ni pesa ya *County*. *So*, Bi Spika makosa ni mingi sana. Tunapongeza hio *Committee* na tunasema tuangalie kinagaubaga vile hizo pesa zimetumika na ni nani *ameauthorize* na itakuwa namna gani. Asante sana Bi. Spika; Hata ile *Madam Speaker* alisema *it was out of order* tulisikia na masikio na tutafanya hivyo. Thank you, very much.

**Hon. Speaker:** Thank you, Hon. Kisini. Hon. Nziva.

**Hon. (Ms.) Nziva:** Asante Bi Spika kwa kunipa nafasi ndio nichangie kwa hii mjadala. Niwape kongole kamati ya barabara kupitia kwa *Vice-Chair* Ho. Irene Mwendu Mbivya kwa kuleta huu mjadala na niseme mimi nimesimama *kuhighlight on Ikombe ward issues* kwa sababu nimeona kidogo tu ni kama hio *status report* haiko vile iko kwa *ground*.

Wakati niliona *advert* ya hii barabara nilienda kuangalia vile mambo inaendelea kwa sababu ni barabara najua *which is No. 4 and the committee noted that only one culvert has been fixed on Kithito-Mangweti road in Kinyata road in Ikombe ward. The report from the department indicated that the installation of culverts and protection works had been done to satisfaction.*

Wakati niliona walikuwa wanataka kuweka *culverts* na hio njia hakuna drainage, niliongea na Katibu na nikamwambia hio pesa kwa sababu imetengwa ya Ikombe na kwa sababu ilikuwa *less than two million* ilikuwa kiwango but nikaamuuliza tufanye *public participation* ndio tuweze kuamend the BQ.

Kupitia kwa PMC na wananchi, tulienda na tukajadiliana kuwa tufanye *heavy grading* na *backfilling* ya *murram* kwa sababu hakukuwa na mahali pa *culvert*. Kwa hivyo Kamati, hakuna mahali *culvert* ilijengwa, kuna *backfilling* na *heavy murraming*. Kwa hivyo ni vizuri muweze kurekebisha kidogo na natumai mambo itakuwa mzuri na niwaunge mkono kusema, *at least* kungekuwa na *equity* watu waweze kupata maendeleo kila mahali na Kaunti ni kubwa na kila mahali tunafaa kupata maendeleo. Asante sana Bi. Spika.

**Hon. Speaker:** Ahsante Mheshimiwa Nziva kwa hayo. Mheshimiwa Ndawa. Na tujaribu kufupisha kwa sababu tunaelewa shida ya barabara ishasemwa tusiwe tunarudia.

**Hon. Ndawa:** Thank you, Madam Speaker. *Nataka nishukuru hio kamati kwa kuleta ripoti ambayo inajieleze yenyewe.* Madam Speaker, *wazungu wanasema 'a sin is a sin no matter who commits a sin.'* And again *wazungu wanasema pia; 'where the Chief's son is circumcised, let the poor mans son be circumcised in the same place.'* Let us not have a place for circumcising kids of the Chief and another for the poor men. What am saying is that we all belong to Machakos County and every ward needs to be given services regardless of who is the leader of that particular area.

Madam Speaker, Article 1 of the Constitution says that the sovereignty of the nation lies with *wananchi* and it further says *wananchi* can exercise that power directly or indirectly. Madam Speaker, indirectly the electorates went to the polling stations and voted a certain candidate to be their representative in the Assembly. The MCA of any particular area represents the interests of the citizens of that particular area and if that area is denied services, it means now we are denying the electorates who elected that particular person.

So, Madam Speaker, it is very unfair if kids of one family are getting meals and another are sleeping without meals. I want to say that whoever is in charge of this department should be able to balance; let every ward get resources, let every ward be treated like the other ward. Madam Speaker, if there is an issue of funds which are not clear, we have institutions which are mandated by the constitution to investigate. Madam Speaker, I call upon the Assembly to invite the relevant Chief Officer to come and shed light on this and incase he is not able to substantiate; let the DCI or EACC be called upon to investigate and if anyone is found culpable of doing he/she is not supposed to do, let that person be taken to jail because that is where he or she belongs.

Madam Speaker, we have limited time and we cannot keep speaking about people not doing their jobs the way they are supposed to be doing it. His Excellency the Governor wherever he is has sent some people to do that job and when they do not do the job we start blaming the Governor but it is another person. So, I want to support the report and say this committee has proved to be doing what it is supposed to be doing; if the other committees can do the same, I am sure we will take Machakos to the next level.

We have been given the highlights of the incoming budget and with the highlights that we were given by the CEC Finance yesterday we heard about Ksh. 1.2 Billion will go to roads. Let us ensure that we see value for that money so that our people can get services. Madam Speaker, the department of roads is interdisciplinary; this means all other departments rely on the department of roads because even if you construct a hospital somewhere without a road you cannot access that hospital.

If you drill a borehole somewhere without a road, people cannot go and fetch the water from that borehole. If you build a school without road, you cannot access so we are saying those who are manning the department of roads should be more serious with their jobs so that other departments can be seen working. Thank you very much, Madam Speaker.

**Hon. Speaker:** Thank you very much, Hon. Ndawa, Hon. King'ori;

**Hon. King'ori:** Thank you, Bi Spika, kwa kunipatia hii nafasi ndio niweze kuongea maneno ya barabara. Sina shida na ripoti kwa sababu ni ukweli na hii shida iko kwenye Kaunti yote ya Machakos kwa sababu niko na *example* nzuri ya Muthwani ambayo barabara ya Kincar road unayojua kuna wakati moja nilirushiwa mchanga na wananchi wakita hio barabara itengenezwe. Nikapigana kabisa na hio barabara ikapatiwa *budget* 2018-2019 ikapatiwa milioni 20.

In 2019/2020 ikapatiwa Ksh. 26 million na saa hii nimeona proposal imekuja imepewa Ksh. 53 million, Bi. Spika. Nauliza sasa juu mimi naishi hapo na nalala hapo ninajua ile kiwango ya kazi imefanywa na ile distance imepewa hio pesa yote haijafika *kilometer* tatu Bi. Spika. Wakati ya kwanza ile kitu ilifanyika kwa hio barabara ilichimba mtaro, ikawacha maji na wananchi wakalalamika. Hii ya pili milioni 26, Bi. Spika ole wangu, ile kitu ilikuja ni tingatinga na mwaka imeisha. Na sasa sijui hio pesa itaenda wapi kwa sababu milioni 26 haijafanya kazi yeyote katika hio barabara.

Saa hii tumeongeza pesa ingine milioni 53 lakini sioni kama kuna kitu ambayo itaendelea na hiyo. Na hio tunaongea kitu haijafika *kilometer* tatu. Hii ni utumizi mbaya wa pesa za umma, Bi. Spika.

Lakini narudi kwa wananchi na najua wanauliza na nyinyi tunafanya kazi wakati gani. Sisi tumefikisha kazi yetu hapo lakini kazi ya mwananchi nayo inanza hapa. Hio kipengee mwezangu amesema ya kwanza ambayo ndio inakupatia *powers* ya kulinda mali yako juu hii pesa si yetu na si ya Gavana; hii ni pesa ile mnalioa *tax*. Hata mkisikia imetoka kwa *national government na unaskia* mkate imeongezwa bei, bodaboda, sijui nini na kama mmesikia juzi mlisikia vitu nyingi zitabadilishwa badilishwa. Ni nyinyi mtalipa hio pesa si watu wengine.

Kwa hivyo hio kipengele inakupatia *powers* kuhakikisha ile kitu imepitishwa kwa bajeti imefanywa. Na hio kipengele pia ndio imekupatia *powers* wakati umeona hatujafanya kazi, unahakikisha tumepelekwa kortini. Na sababu Gavana na serikali ambayo iko inajua ukweli mwananchi hana hio nguvu ndio sababu inapita njia ya mkato ambayo so ya halali na sasa



nauliza nyinyi wananchi. Kama mimi siwezi peleka serikali kortini hii ni wajibu wenu mshikane ndio muweze kutupeleka kortini kama serikali ya kaunti ya Machakos haifanyi kazi.

Na hivyo ndio katiba inasema kwa sababu sisi tumewekwa na nyinyi katika kipengele ya 176 kama sijakosea ambayo inasema tutaunga serikali ambayo itakuwa ni ya chini ambayo sisi tuko ambayo itakuwa na *County Assembly* na *Executive* ambayo inaongozwa na Gavana, *Madam Speaker*.

Kwa hivyo sisi hatuwezi jipeleka kortini; wananchi ndio mnafaa mshikane na timu yenu mpeleke serikali ya kaunti kortini kwa utumizi mbaya wa pesa za umma. *That is how it should be*. Hii ripoti ya *Auditor General* (??) ambayo inasemekana ni ya ukweli kabisa lakini kuna mahali nimeona nimechanganyikiwa Bi Spika, si kwa ubaya lakini nimeona kwa zile vitu nilikuwa nataka, nilikuwa naomba---

**Hon. Speaker:** Do we have a report by Auditor General?

**Hon. King'ori:** Nasema kuna ripoti ambayo imesemekana imetoka kwa Auditor General Bi. Spika.

**Hon. Speaker:** In this report? It is the Controller of Budget.

**Hon. King'ori:** Yes, I am sorry Madam Speaker its just a mix up; *naomba radhi. Lakini nimeona wakati tinga inaripotiwa ile kazi imefanya nimeona imefanya 40 per cent lakini ile pesa imetumika ni over ile tulikuwa tumepitisha kwa budget. Nauliza ilitumika wapi kwa sababu kama matingatinga haikufanya kazi na pesa ilitumika, ilitumika namna gani? Hio ndio swali mwananchi anafaa aulize.*

*Ya pili; unasikia kazi ambazo zinafanywa na haziishi na pesa ya wananchi imetumika. Hio pesa ilienda wapi? Hio ndio swali wananchi wanapsawa waulize. Kwa hayo machache na mengi, nasema asanteni.*

**Hon. Speaker:** Thank you, *Mheshimiwa King'ori. Mheshimiwa Kituku.*

**Hon. Kituku:** Bi Spika Asante. Unajua kila moja amesikia *ameboeka* juu ya hizo *mastori*. Sio stori nzuri. Bi. Spika, mimi naomba kwa uongozi wako utusaidie juu sasa tuko mwisho na juu sisi ni kama korti hatuwezi kupiga hio hatua nyingine juu kulingana na yale maelezo ambayo bunge imetoa, ni wazi kwamba pesa yetu imepotea. Na ripoti tunapatiwa ni riport ambayo pia iko *mixed up*.

Bi Spika ukiangalia hio ripoti, utaona zile pesa tunapata kwa mfano KRB hizo utaona zimefanya kazi lakini zetu kama *County* hata ingawa hizo pia ni zetu, zile ambazo zinatuhusu ndani ndani, hakuna kazi zinafanya. Utaona nyingi ni *project stalled*, kwa *percent* kumi, tano na shida ni nini? Tunapatiana pesa lakini haifanyi kazi. Kwa mfano, *most of the buidlings, for instance, commcerical development stalled stalled at 10 per cent, community recreation centers 6.5 per cent, office block 6.5 per cent* kwa sababu ni gani na kila mara ile ripoti tumekuwa tukishinda kuambiwa ni kutafanywa *tendering* tena lakini hio ni mchezo juu hakuna wakati hio kitu inafanyika.

Barabara za KRB juu pesa huwa iko tayari hata ninakuhakikishia hii pesa ya *Climate change* hakuna pesa itabaki itakuwa inatumika haraka kwa sababu pesa hio iko tayari. Ukiangalia pesa ya World Bank, zile *areas* ambao zimefanyiwa kazi na hio pesa, kazi

inafanyika lakini ile pesa yetu sisi kama kaunti hakuna kitu inafanya. Na juu kila mmoja hapa kama Mheshimiwa amekubali, hatutaendelea kulia hapa. Itabidi hata kama ni the General Oversight Committee Bi. Spika kwa uongozi wako utusaidie vile tunaweza ita *department* ituelezee wazi after hio tuchukue *the next* hatua juu Mheshimiwa Spika, aki ya Mungu tunaendelea vibaya na wananchi wanaumia---

**Hon. Speaker:** *Mheshimiwa Kituku*, that is out of order. Please do not use those words.

**Hon. Kituku:** I withdraw.

**Hon. Speaker:** Thank you.

**Hon. Kituku:** Madam Spika, ili tuweze kuchukua hatua ambayo itaweza kusaidia hii kaunti yetu na tuweze keundelea na mbele. Na kulingana na *mood* ya *House* Waheshimwa ni kama kuna mahali wamefika na tuko tayari kufanya chochote. Asante.

**Hon. Speaker:** Shukrani Mheshimiwa Kituku. I *call upon the mover of the motion to reply*.

**Hon. (Ms.) Mwende:** Asante sana Bi. Spika na Waheshimiwa wabunge kwa *contributions* zenu na asante pia kwa wananchi kwa *patience* yenu ya kutungoza tuongee mambo zetu na pia inayowahusu na tunawashukuru. *So*, Bi. Spika, ugatuzi uliletwa ndio kila kaunti ipate maendeleo, na niko na uhakika kwamba hakuna Mheshimiwa angetaka umechanguliwa na maendeleo hayataletwa kwako. Ungeambiwa hivyo *before* hata ungetaka kusimama; otherwise ulisimama *because* ulitaka kuletea *development* kwa watu wako.

Na committee recommendations according to Article 10(2)(b), inaongea maneno ya *inclusivity, equality, equity and non-discrimination*. Na tunaomba *county government*; hii *county* yote ni ya Machakos, si ya Waheshimiwa wachache, ni ya waheshimiwa wote *59 plus one*.

*So* tunaomba maendeleo ikuwe kwa kila moja ndio pia wewe ukitoka hapa kama Mbunge ujivunie kwamba *the Governor of the county government of Machakos was able to bring equality in terms of development* na si kupendelea wengine maanake hata kama ulichaguliwa kwa chama ingine na wewe ni wa chama yake, bado maendeleo ni ya watu wa Machakos si ya watu wa chama yake peke yake.

*Otherwise* nashukuru sana na nashukuru pia kwa mchango wenu na pia Bi. Spika *and the office of the Clerk for the coordination and efforts to make the committee in the Assembly work well. Even our Clerk Asistants, I thank you so much for the efforts you take to write the reports and we are grateful. Thank you.*

**Hon. Speaker:** Thank you, Hon. Irene.

*(Question put and agreed to)*

## ADJOURNMENT

**Hon. Speaker:** Hon. Members, at this point the sitting of the House is adjourned to resume on 29th June, 2021 at 10.00 a.m. Have a good afternoon Hon. Members.

The House rose at 2.38 p.m.